Kama unataka kujifunza zaidi njia ya Mkristo wa kweli anavyopaswa kuishi, basi ni lazima ujifunze Biblia. Ili kukusaidia; Kanise la Christadelphian Bible Mission limechapisha kijitabu kuhusu mafunzo ya Biblia kaitka somo hili muhimu.

Lina itwa <u>Kuishi katika Ukweli.</u> Unaweza kupata nakala kutoka Kanisa la Christadelphian, au kutoka anuani iliyoandikwa katika kijitabu hiki.

CBM Publishing
32 Blenheim Road, Far Cotton
Northampton, England. NN4 8NW

ISBN 1 902059 18 -2
Registered Charity Number: 248979 / 1020558
Company Number: 2796412
Telephone +44 (0) 1604 765068
Facsimile +44 (0) 1604 463578
Email: CarlHinton@hotmail.com
Web: http:\\www.bedford-ecclesia.org.uk/Swahili

9781902059181

# KITABU-MWALIMU WA KRISTADELFIANI

The Christadelphian Instructor

Kufasiri: Simon Uswegi
Muumba: Carl Hinton

Tena:


| | |
|---|---|
| 1 902059 00 - X | Matayarisho ya Ubatizo |
| 1 902059 01 - 8 | Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 1-4 |
| 1 902059 02 - 6 | Ukimwi |
| 1 902059 03 - 4 | Mshitaki Wenu Ibilisi |
| 1 902059 04 - 2 | Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 5-8 |
| 1 902059 05 - 0 | Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 9-11 |
| 1 902059 06 - 9 | Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 12-15 |
| 1 902059 07 - 7 | Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 16-19 |
| 1 902059 08 - 5 | Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 20-23 |
| 1 902059 09 - 3 | Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 24-27 |
| 1 902059 10 - 7 | Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 28-31 |
| 1 902059 11 - 5 | Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 32-36 |
| 1 902059 12 - 3 | Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 37-40 |
| 1 902059 13 - 1 | Ufunuo Mlango wa Kwanza |
| 1 902059 14 - X | Ni kweli Yesu Kristo alishuka kutoka mbinguni? |
| 1 902059 15 – 8 | Nyimbo za ndugu wa Kristo |
| 1 902059 16 – 6 | Ufunuo Mlango wa Pili |
| 1 902059 17 – 4 | Katiba ya Makanisa |
| **1 902059 18 – 2** | **kitabu-mwalimu wa kristadelfiani** |

(3) KUKUMBUKA DHABIHU YA KRISTO

"Nalipokea kwa Bwana liniliyowapa nanyi, ya kwamba usiku ule Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. Na vivi hivi baada ya kukitwaa kikombe, akasema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu" (1 Kor. 11:23-25).

"Katika siku ya Kwanza ya juma, … wanafunzi walikusanyika pamoja ili kuumega mkate""(Matendo 20:7).

"Msiache kukusanyika pamoja" (Ebrania 10:25).

---



KITABU-MWALIMU
WA
KRISTADELFIANI

MASWALI NA MAJIBU JUU YA KWELI NAYO
YAMEDHIHIRIKA KATIKA MAANDIKO MATAKATIFU
PAMOJA NA MAFUNGU MADOGO YA MANENO YA BIBLIA
YALIYOJAA TELE
MWISHONI KWA KARIBU KILA JIBU
NA
ROBERT ROBERTS

Kwanza kilichapishwa 1886
(kilirudiwa tena kwa lugha ya kiingereza 1954 na 1974)

Toleo jipya kwa kiswahili 1998.

---

YALIYOMO

---

**UTANGULIZI** *(Foreword)*

MARUDIO YA 1954

Kitabu-Mwalimu wa Kristadelfiani kilicho andikwa na Ndugu Robert Roberts katika mwaka 1886, kimeshiriki sehemu muhimu sana katika kuwaelimisha vijana wetu kwa kujua Maandiko, kwa pande mbili, yaani, katika Shule ya Jumapili (Sunday School) na sehemu binafsi, na tangu wakati huo, kimeendelea kuwa na matakwa tele.

Kwa jinsi wakati unavyopita, yamefanyika mabadiliko kwa mtazamo wa elimu kwa ujumla, katika utaratibu na jinsi ya kufundisha Shule zetu za Jumapili. Shule zetu nyingi kwa sasa zimejitengeneza vizuri zaidi, pamoja na mafunzo nyuma yake yaliyopokelewa hapo awali kwa maneno yaliyodokezwa katika kuongoza Shule ya Jumapili yaliyokuwamo hapo kwanza ndani ya Kitabu hiki hayahitajiki tena. Shule zetu nyingi masomo yake yanakuwa katika wazo la kuchunguza kwa makini kutoka kwenye muhutasari wa mafunzo ya muhimu yalioyopanuliwa zaidi kipindi chote cha uhai wa Shule ya Jumapili, ambayo yamewekwa msingi wake kwenye historia ya Mungu akijishughulisha na mwanadamu kama ilivyodhihirika katika Agano la Kale na Jipya, pamoja na msisitizo mahususi juu ya maisha yake Bwana Yesu Kristo na kazi yake. Hii inafuatiwa na kozi ya wanafunzi walio wakubwa kwa umri katika mwelekeo wa mafundisho ya KWELI na kuwatayarisha kwa ajili ya ubatizo. Waalimu wetu, nao pia, wanafaida kwa jambo moja moja la maelezo ya masomo, yaliyo katika muhutasari utoao msaada wa maana sana kufundisha, misaada ya kufunza, na vyanzo vya nyongeza kwa habari ya kazi zao.

Kwa hali ya namna hii inaweza kuulizwa, "Je! Kitabu-Mwalimu kwa sasa kinatumika kwa kusudi la maana katika kuwaelimisha watoto wetu?" Kwa imani yetu ni ndiyo, na isitoshe kina sehemu muhimu kujaza panapohitajika. Kinachohitajika kipo katika mafundisho namna wanafunzi wetu jambo wanaloliangalia sana, hasa juu ya elimu ya msingi kwa tunachikiamini, kuonyesha uhusiano wao muhimu na "kuthibitisha" mbele yao hasa "sababu za kweli za Maandiko Matakatifu". Kitabu Mwalimu kinatimiza jambo hili. Kina mkusanyiko wa Maandiko mengi ya historia ya kweli kwa azimio linaloendelea la Mungu kwa mwanadamu, yanasisitiza uhusiano wao, na kuwaleta watu kwenye jambo lililokusudiwa tangu zamani katika maisha na kazi ya Bwana Yesu Kristo. Kila moja ya KWELI hizi zimeonyeshwa kuwa zimo katika Neno la Mungu kwa mafungu ya maneno yaliyotolewa ili kusaidia ukweli huu. Kujifunza kwa akili na uangalifu wanafunzi wetu hiki Kitabu-Mwalimu – hasa walio wakubwa, washirika wa jumuia ya Vijana walio na rika lililo sawa, wakiwa chini ya mwongozo wa upole wa huyo mfunzi aliyemzoefu au kiongozi anayehesabika kuwa ni mwenye kuelimisha katika nuru, huwatayarisha na kuwatia moyo ili wautii mwaliko wa Mungu kwa njia ya Yesu Kristo.

Tunapenda kutia mkazo maneno "jifunze kwa akili na uangalifu kitabu-mwalimu". Hii inahusisha zaidi mno, kuliko kukumbusha tu "mathibitisho" kwa watoto kazi ya nyumbani. Pamoja na mafunzo mengine magumu (kama asili ya dhabihu ya Kristo) maelezo ya maana na ufafanuzi unaweza kuhitajika, naye mwalimu yampasa kuwa tayari kusoma jambo linalozungumziwa na kulitoa. Wanafunzi watiwe bidii ya kujadili habari hizi, kutaja yaliyo magumu, kupima maneno yanayoonekana kuwa na upinzani yanayoweza kuletwa na wenye imani tofauti na yetu, na hivyo kushika sana sura hizi za mafunzo ya Imani.

Ingawa wakati mwingine lawama zaweza kuwepo, yapo mengi ya kusema kwa upande wa kufundisha kwa moyo "mathibitisho" ya Maandiko na kuwakumbusha wanafunzi ya kuwa wanjifunza elimu ya Mungu juu ya mafunzo ya msingi. Sio lazima kwa kila ushuhuda uliomo katika Kitabu-Mwalimu kufundisha kwa moyo, mara nyingi ushuhuda umetolewa kutoka sehemu tofauti-tofauti za Maandiko ili kuonyesha mafundisho yaliyomo katika Neno – yanayofaa zaidi yachaguliwe ili kwamba yafundishwe kwa moyo. Yasomwe kwa 'moyo' (yaani, kwa kutaka kufahamu) na sio bila 'akili'.

Uwezo wa kupenda kujifunza kwa moyo vijana kwa upana utajulikana, nasi tutashauriana kwa faida inayodumu upande wa vijana ikiwa tutawazoeza vya kutosha katika kufahamu na kujifunza kwa moyo Maandiko katika ujana wao. Kitu tusichohitajika ni kuwawekea mipaka kwa "mathibitisho"; kuna mafungu mengi ya maneno katika Zaburi, Manabii, katika Injili na Nyaraka, ambayo kwa sababu ya uzuri wake wa kuvutia yatawapatia urithi wa akili na thamani ambayo faida yake haihesabiki kwa maisha yao ya baadaye.

Kwa kufuata mfano wa mafunzo yaliyo katika Kitabu-Mwalimu, toleo hili jipya litawafaidisha wasomaji wa Kiswahili wa hapa Africa ya Mashariki na kwingineko baraka zake Mungu katika kujua aliyokusudia tangu zamani.



"Kwa maana kwa yeye sisi sote tumepata njia ya kumkaribia Baba katika Roho mmoja" (Mstari wa 18).

"Maana amesema, sitakuacha wala kukupungukia; hata twathubutu kusema: Bwana ndiye anisaidiaye, sitaogopa; mwanadamu atanitenda nini" (Ebrania 13:6,7).

"Bwana atakuwa ngome kwake aliyeonewa, naam, ngome kwa nyakati za shida. Nao wakujuao jina lako wakutumaini wewe" (Zaburi 9:9,10).

"Fadhili za Bwana zina wamchao tangu milele hata milele: kwa wale walishikao agano lake, na kuyakumbuka maagizo yake ili wayafanye" (Zaburi 103:17,18).

"Maana hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, Mwokozi wetu Yesu Kristo" (2 Petro 1:10,11).

166) Ni msaada upi maalum ambao humsaidia kuelekea kwenye Ufalme wa Mungu?

Kanuni tatu amepewa anayeamini; zitamsaidia katika jukumu lake kubwa la "kufanya imara kuitwa kwake na uteule". Ya kwanza ni

(1) Kusoma Neno la Mungu;
(2) Sala;
(3) Kuikumbuka dhabihu ya Kristo kwa kuumega mkate na kunywa divai kwenye siku ya kwanza ya kila juma.

(4) KUSOMA MAANDIKO.

"Neno lako ni taa ya miguu yangu na mwanga wa njia yangu … Neno lako nimeliweka moyoni mwangu nisije nikakutenda dhambi" (Zaburi 119:11,105).

(5) SALA.

"Ombeni bila kukoma" (1 Wathesalonike 5:17).

"Kwa kila jambo kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, na haja zenu na zijulikane na Mungu, na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu" (Wafilipi 4:6,7).

"Na kila asikiaye maneno yangu asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, ikaanguka; nalo anguko lake likawa kubwa" (Mathayo 7:26).

164) Je! kuna msamaha kwa wale ambao wamejitoa ili waitii injini, na halafu wanaweza kushindwa kutii kwa kikamilifu maagizo ya Kristo?

Ndiyo upo msamaha; kama ingekuwa sivyo, basi pasingekuwapo mtu wa kuweza kuokolewa. Lakini msamaha hutegemea kukiri kwetu na kuziacha dhambi zetu, na jinsi tunavyo wasamehe wengine; nao msamaha hutolewa tu kwa kazi ya upatanisho wa Kristo.

"Kama wewe, Bwana, ungehesabu maovu, Ee Bwana, ni nani atasimama? Lakini kwako kuna msamaha" (Zaburi 130:3-4).

"Kama tukitembea katika nuru … damu ya Yesu Kristo yatusafisha dhambi zetu zote" (1 Yohana 1:7).

"Mtu akitenda dhambi, tunaye mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki" (1 Yohana 2:1).

"Tukiziungama dhambi zetu zote, yeye ni mwaminifu kutuondolea dhambi zetu kabisa" (1 Yohana 1:9)

"Yeye yu hai sikuzote ili awaombee (atuombee) (Ebrania 7:25); na Warumi 8:34). "Ikiwa ninyi hamtawasamehe watu, wala Baba yenu naye hatawasamehe makosa yenu" (Mathayo 6:15).

165) Ni kwa njia gani Mungu anatusaidia kushika amri zake na kupata wokovu wake?

Watoto wake wanayo faida kubwa ya kushirikiana naye na pamoja na Mwana wake, wa wana njia ya kumkaribia Mungu kwa njia ya sala kupitia Kristo. Ameahidi kuwa kamwe hatawaacha wala kuwatupilia mbali; anakuwa kimbilio wakati wa taabu, na kuwaongoza katika maisha. Upendo wake, rehema na amani Yake huwapa wao, na vile vile, wakiwa ni waaminifu, atawaruzukia kuingia kwa uingi katika Ufalme Wake.

"Kweli ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana Wake, Yesu Kristo" (1 Yohana 1:3)

"Ninyi mliokuwa mbli hapokwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo" (Efeso 2:13).



Tunaamini kwamba kwa baraka zake Mungu hiki Kitabu-Mwalimu kitaendelea na kazi yake njema ya kuwasaidia vijana wetu kuelewa Neno la Mungu, na kuwatayarisha kuitika kwa akili na upendo kwa neema aliyoitoa kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.

Kimetafsiriwa CBM Mwanza.
1998

MWALIMU
WA KRISTADELFIANI
*(The Christadelphian Instructor)*

**MAANDIKO** *(Preparation)*

Kupata wokovu itahitajika kuwa na elimu ya kutosha ya kumjua Mungu na Yesu, mwana wa Mungu.

1) Ni wapi tunaweza kupata elimu hii?

Katika Maandiko Matakatifu, yamejulikana katika siku zetu kuwa ni Biblia.

"Tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu yanayoweza kukuhekimisha hata ukapata wokovu kwa njia ya imani kwa Kristo Yesu" (2 Tim. 3:15).

"Yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini" (Rum. 15:4).

"Kufafanusha maneno yake kwatia nuru: na kumfahamisha mjinga" (Zab. 119:130).

"Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu" (Zab. 119:105).

2) Biblia ni kitu gani?

Neno Biblia maana yake ni KITABU. Ni kitabu kilicho andikwa kwa uongozi wa Mungu akitenda kazi ndani ya manabii na mitume walioishi zamani huko Israeli. Waliishi katika nyakati tofauti na kuandika kwa kutofuata mashauri ya mtu; bali Roho wa Mungu ndiye aliyewaongoza wote, na kuwawezesha kuwajulisha watu nia ya Mungu katika historia, amri zake na unabii, kwa sababu hiyo basi hii Biblia ingawa ina vitabu vingi, ni Neno la Mungu moja tu.

"Kila andiko lenye pumzi ya Mungu la faa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki" (2 Tim. 3:16).

"Mungu ambaye alisema na baba zetu zamani katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema nasi katika Mwana" (Heb. 1:1).

"Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu" (2 Pet. 1:21).

"Neno lako ndiyo kweli" (Yoh. 17:17).



(9) Efe. 4:25.
(10) Fil. 2:15.
(11) Luka 14:11-13. Fil. 4:4; 1 Thes.5:8-10.
(12) Fil. 4:8

162) Unaweza kutaja katika mambo yasiyostahili kuyafanya?

(1) Ubwana mkubwa hautakiwi;
(2) kurudisha baya kwa ubaya;
(3) tusilipe kisasi bali tuipishe gadhabu;
(4) haupashwi kutoa sadaka zetu ili tutazamwe na watu wala mkono wa kushoto usijue mkono wa kuume unafanya nini;
(5) hatutakiwi tuhangaike ili tuwe matajiri wala kupenda au kuufuatisha ulimwengu;
(6) tusilaani, au laumu kwa laumu, bali tubariki;
(7) tusing'unike au kuhukumu;
(8) tusiwe na hasira, gadhabu, uchungu, au maongezi yasiyo faa;
(9) tusiwe wavivu kulipa madeni yetu;
(10) tusiwe wenye kuteta au kusema dhambi za watu wengine mpaka tuwe tumesema nao kwanza;
(11) tusiwe na hatia ya unajisi, ulevi, tamaa ya kupata, gadhabu, wazushi, wafitini, chuki, majivuno, husuda au wivu, kijicho au maneno ya kipumbavu.

(1) Math.23:11; Yohana 13:13-17.
(2) Rumi 12:17.
(3) Rumi 12:19-20.
(4) Math. 6:1-4.
(5) 1 Tim.6:8.
(6) 1 Pet. 3:9
(7) Yak. 4:11; Math. 7:1; Fil. 2:14.
(8) Efe. 4:31; 1 Pet. 2:1
(9) Rumi 13:7-8.
(10) Math. 18:15; Yak. 5:19,20.
(11) Efe. 5:3-4.

163) Je! injili pamoja na ubatizo vyaweza kutuokoa ikiwa sisi sio watii wa hizo amri?

Hapana; kuamini kwetu injili na ubatizo itakuwa tu ni kwa kuhukumiwa kwetu kama tukiishi maisha ya uasi kwa amri za Kristo. Wale ambao ni watii wa maagizo yake watakuwa ni miongoni mwao waliobarikiwa.

"Heri wazishikao amri zake; na kuwa na haki ya kuuendea mti wa uzima, na kuweza kuingia mjini kwa milango yake" (Ufunuo 22:14).

"Enendeni ulimwenguni mkawafundishe watu wa mataifa yote, mkawabatize … na kuwaagiza kuyashika yote niliyowaamuru ninyi" (Mathayo 28:19-20).

"Ninyi ni rafiki zangu mkitenda yote niwaamuruyo" (Yohana 15:14).

159) Tunaweza kupata wapi hizi amri za Kristo?

Katika habari ya mafundisho ya Kristo yaliyomo ndani ya injili, yaliyojulikana sana kuwa ni Hotuba ya Mlimani (Mathayo sura ya 5, 6 na 7), na katika maandishi ya mitume wake.

160) Amezifupisha vipi hizi amri?

Alitamka amri kubwa mbili, (a) wajibu kwa Mungu, na (b) wajibu kwa mwanadamu, kama ifuatavyo:

"Yesu alisema, Umpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili yako yote. Hii ndiyo amri ya kwanza iliyo kubwa, na ya pili inafanana nayo. Mpende jirani yako kama nafsi yako" (Mathayo 22:37-39).

161) Unaweza kutaja baadhi ya amei za Kristo na mitume wake?

(1) Tumpende Mungu na Kristo;
(2) tuwatendee mema watu wengine kama tunavyopenda kufanyiwa sisi;
(3) kupendana;
(4) kushirikiana na watu katika huzuni na furaha;
(5) kuwapenda hata maadui na kuwabariki wao wanaotulaani, na kufanya mema hata kwa hao wanaotuchukia, na kuwaombea wanaotutendea vibaya;
(6) kuwa tayari kwa kazi yo yote njema, kuwapa wanaotuomba, kuwahurumia wanaoteseka;
(7) kuwa waaminifu hata kwa mabwana waliyo wabaya;
(8) kuomba kila siku na kwa kila jambo kushukuru;
(9) kusema ukweli daima;
(10) kutokuwa na lawama wala mawaa;
(11) kuwa wapole, mashujaa, wenye furaha, wakarimu na wazima katika imani;
(12) kufuata yaliyo ya kweli, yaliyo ya heshima, safi, ya haki, yenye upendo na yaliyo na taarifa njema.

(1) Math. 22:37; Luka 10:27.
(2) Math. 7:12.
(3) Yohana 13:34.
(4) 12:15.
(5) Luka 6:27-28; 1 Petro 3:9; Math. 5:44.
(6) Tit. 3:1; Math.5:42; Rumi 12:13
(7) 1 Tim.6:1-2.
(8) Luka 18:1; Ef.5:20;



3) Biblia imegawanyika sehemu ngapi?

Katika sehemu mbili: Agano la Kale na Jipya. Agano la Kale liliandikwa na Musa na Manabii, waliomfuata baadaye. Agano Jipya liliandikwa na Mitume.

4) Taja baadhi ya watu zaidi waliotumiwa na Roho wa Mungu kuandika Biblia?

Musu, Yoshua, Samueli, Daudi, Sulemani, Isaya, Yeremia, Ezekieli, Danieli, na manabii wengine katika Agano la Kale; Mathayo, Marko, Luka, Yohana, Paulo, Yakobo, Yuda, na Petro katika Agano Jipya.

5) Zaidi ya kipindi cha wakati gani utunzi wa Biblia ulipanuka?

Agano la Kale lilianzwa na Musa karibu miaka 1,400 kabla ya Kristo, nalo lilimalizika na Malaki miaka 400 kabla ya Kristo. Agano Jipya liliandikwa katika zama za uhai wa Mitume, baada ya ufufuo na kupaa kwa Kristo, zaidi ya miaka 1900 iliyopita.

6) Biblia ina vitabu vingapi?

Biblia ina vitabu sitini na sita: therathini na tisa katika Agano la Kale, na ishirini na saba katika Agano Jipya.

**MUNGU** *(God)*

7) Biblia yatufundisha nini kuhusu Mungu?

Ya kuwa Mungu ni mmoja, Muumba wa milele wa vitu vyote naye ni Baba wa Bwana Yesu Kristo.

"Yupo Mungu mmoja, na mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, mwanadamu Kristo Yesu" (1 Tim. 2:5).

"Sikia, Ee Israeli, Bwana Mungu wetu ndiye Bwana mmoja" (Kumbukumbu 6:4).

"Mimi ndimi Bwana: hapana mwingine zaidi yangu mimi hapana Mungu" (Isaya 45:5).

"Lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu; aliye BABA, ambaye vitu vyote ni vimetoka kwake" (1 Kor. 8:6).

"Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana Yesu Kristo" (2 Kor. 1:3).

"Tangu milele na milele ndiwe Mungu" (Zaburi 90:2).

8) Biblia yatufunulia ni sifa gani aliyonayo Mungu?

Ni kwamba yeye ni mwema, lakini anataka watu watii sheria zake; ni mwenye upendo na huruma, lakini hatavumilia uasi na makosa, ni mwenye kusamehe, lakini ni Mungu mwenye wivu, kwa utukufu, na ukuu wa Jina lake. Yeye Mungu ni mtakatifu, ambaye macho yake hayaangalii palipo na dhambi. Ni mwenye busara, wa kweli na mwaminifu, lakini ataangamiza yote yaliyopotoka. Ni mwenye haki na kweli na mkamilifu – chemchemi ya upendo na kisasi; muumba wa uhai (uzima) na mauti; mwanzo wa kuanzisha rehema na hukumu ya kuangamiza. Yeye ni wa milele, asiyebadilika, asiyechunguzika, asiye na kikomo, ni mwenye utukufu na sifa kuu na uweza wa ukuu – Mfalme asiyepatikana na mauti, mmiliki mbingu na dunia, ambaye pekee astahiliye kuabudiwa.

Kutoka 20:5 na 6; Zaburi 103:8-13; Habakuki 1:13; Zaburi 5:5-6; Yeremia 10:10-13; Kumbukumbu 32:4; 1 Yohana 4:7,8,16; Ebr. 10:30-31; Kumbukumbu 32:39; 1 Timotheo 1:17; Zaburi 145:3; 147:5; Mwanzo 14:19-22; Zaburi 115:1; Yuda 25.

9) Je, Mungu amejifungia mbinguni ingawa anaishi huko?

Hapana: Yupo kila mahali na hakuna kinachoweza kujificha kutoka kwenye fahamu zake.

"Je, mtu yeyote aweza kujificha mahali pa siri, nisimwone? Asema Bwana. Je! Mbingu na nchi hazikujawa nami? Asema Bwana" (Yeremia 23:34).

"Wale hakuna kiumbe kisichokuwa wazi mbele zake, vyote vi utupu na kufunuliwa machoni pake yeye aliye na mambo yetu" (Ebr. 4:13).

"Ee Bwana, umenichunguza na kunijua, wewe wajua kuketi kwangu na kuondoka; Umelifahamu wazo langu tokea mbali, umepepeta kwenda kwangu na kulala kwangu; … maana hakuna neno ulimini mwangu usilolijua kabisa, Bwana" (Zab. 139:1-4).

10) Ni kwa njia ipi Mungu yupo kila mahali ikiwa yuko mbinguni?

Mungu yupo kila mahali kwa njia ya Roho wake.

"Waipeleka roho yako, wanaumbwa" (Zaburi 104:30)

"Niende wapi nijiepushe na roho yako? Au niende wapi niukimbie uso wako? Kama nikipanda mbinguni wewe upo; nikifanya kitanda changu kuzimu (kaburi) wewe uko" (Zaburi 139:7-8).



155) Ni tendo lipi la utii ambalo ni la kwanza analolitaka Mungu?

Ubatizo: kwa ajili ya ondoleo la dhambi.

"Tubuni na mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi" (Matendo 2:38).

"Petro akawaamuru wabatizwe kwa jina la Bwana" (Matendo 10:48).

"Aaminiye na kubatizwa ataokolewa" (Marko 16:16).

"Inuka, ubatizwe na uoshe dhambi zako" (Matendo 22:16).

156) Ubatizo ni nini?

Ni kuzama ndani ya maji mengi mwili wote, ishara ya maisha yetu ya kale pamoja na dhambi zake yanazikwa, na kufufuliwa katika maisha mapya: kama Kristo alivyokufa, na kuzikwa kisha akafufuka tena, hivyo nasi kwa kubatizwa ni tendo la kufuata mfano wake.

"Tunazikwa pamoja naye (Yesu) kwa ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka kutoka wafu kwa utukufu wa Baba nasi basi tuenende katika maisha mapya" (Rumi 6:4).

"Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo, na katika huo mkafufuka naye, kwa kuziamini nguvu zake Mungu aliyemfufua katika wafu" (Kol.2:12).

157) Ubatizo unatufanyia kitu gani kingine?

Unatuunganisha na Kristo kama ndugu zake, na kujenga tena uhusiano kati yetu na Mungu kama watoto wake.

"Ninyi nyote ni watoto wa Mungu kwa imani iliyo kwa Kristo Yesu. Maana kama wengi mlivyobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo … wote ni wamoja katika Kristo Yesu" (Wagalatia 3:26-29).

**AMRI ZINGINE ZA KRISTO**

*(The Commandments of Christ)*

158) Je! imani pekee na Ubatizo waweza kutuokoa?

Hapana: utii kwa amri zote za Kristo pia ni lazima.

"Kuamini ni kuwa na uhakika wa mambo yanayotumainiwa, bayana ya mambo yasiyoonekana" (Waebrania 11:1).
"Imani huja kwa kuamini kwa kusikia, na kusikia neno la Mungu" (Rumi 10:17).

152) Tuamini kitu gani kabla ya kuweza kuokolewa?

Yatupasa tuiamini injili aliyoihubiri Yesu na mitume wake.

"Enendeni dunianі kote mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye ma kubatizwa ataokoka" (Marko 16:16).

"Injili ni uweza wa Mungu uletao wokovu" (Rumi 1:16).

153) Injili ni nini?

Neno "injili" maana yake habari njema: ni habari njema zilizotamkwa na Kristo na Mitume ambazo ni mambo yanayohusu Ufalme wa Mungu na jina la Yesu Kristo.

"Yesu alikuja Galilaya akihubiri injili ya ufalme wa Mungu" (Marko 1:14).

"Yesu alipita kila mji na kijiji akihubiri na kuitangaza habari njema ya ufalme wa Mungu" (Luka 8:1).

"Naye akawaambia, imenipasa kuihubiri injili ya ufalme wa Mungu katika miji mingine pia, maana ndiyo sababu nalitumwa" (Luka 4:43).

"Wakamwamini Philipo alipozihubiri habari njema za ufalme wa Mungu na jina lake Yesu" (Matendo 8:12).

"Nao (Mitume) wakahubiri injili katika vijiji vingi vya Wasamaria" (Matendo 8:25).

"Mimi (Paulo) nimekwenda nikihubiri ufalme wa Mungu" (Matendo 20:25).

"Paulo akakaa kwa muda wa miaka miwili mizima katika nyumba yake aliyoipanga … akihubiri ufalme wa Mungu, na kufundisha mambo yale yanayomhusu Bwana Yesu Kristo" (Matendo 28:30).

154) Jambo lingine la lazima kwa wokovu mbali ya imani ni nini?

"Matendo" – yaani ni utiifu kwa maagizo ya Mungu kama yalivyofundishwa na Yesu.
"Imani isiyo na matendo imekufa. Kwa matendo imani inakamilika … Kwa matendo mtu anahesabiwa haki, na sio kwa imani tu" (Yakobo 2:20-24).



**ROHO WA MUNGU** *(The Spirit of God)*

11) Ni uweza wake au nguvu ambayo ameitumia kwa kuumba mbingu na nchi na kufanya vitu vyote viwepo na sisi tunaishi na kutembea na kuwapo.

"Roho ya Mungu imeniumba" (Ayubu 33:4)

"Kwa roho yake amezipamba mbingu" (Ayubu 26:13)

"Watuma roho yako nao wanaumbwa" (Zaburi 104:30)

"Kwa neno la Mungu mbingu ziliumbwa" (Zaburi 33:6)

"Umeziumba mbingu na nchi kwa uweza wako mkubwa" (Yeremia 32:17)

"Hapo mwanzo, Roho ya Mungu ilitulia juu ya uso wa maji" (Mwanzo 1:2)

"Ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu" (Mdo. 17:28).

"Kama akijikusanyia roho yake na pumzi yake, wote wenye mwili wataangamia pamoja, mwanadamu atarudi mavumbini tena" (Ayubu 34:14-15)

12) Je kweli zote hizi zinakupa fundisho lolote kuhusiana na mwenendo wako?

Ndiyo. Nafundishwa kwamba siku zote nipo mbele za Mungu ingawa siwezi kuona na ya kuwa daima ananiona (hata nikiwa gizani) ingawa siwezi kumuona Yeye. Hakuna kinachoweza kutokea pasipo Yeye kujua. Hata mawazo yangu yaliyo ya ndani kabisa na makusudio ya moyo Yeye huyaona, ingawa nitataka kuyaficha.

"Mungu ananiona" (Mwanzo 16:13).

"Wale hakuna kiumbe kisichokuwa wazi mbele zake" (Ebr. 4:13).

"Umelifahamu wazo langu tokea mbali … maana hamna neno ulimini mwangu usilolijua kabisa Bwana. Giza nalo halikufichi kitu … giza na mwanga kwako ni sawasawa" (Zaburi 139:2,4,12).

"Ni mwenye kutambua mawazo na makusudi ya moyo" (Ebr .4:12)

## MALAIKA *(Angels)*

13) Malaika ni nani?

Ni viumbe wenye utukufu na nguvu wanaotumwa na Mungu kufanya kazi mbalimbali ulimwenguni.

"Mhimidini Bwana enyi malaika zake, ninyi mliohodari (nguvu), mtendao na kutimiza neno lake, mkisikiliza sauti ya neno lake" (Zaburi 103:20).

"Malaika Gabrieli alitumwa na Mungu hadi Galilaya katika mji unaoitwa wa Nazareti" (Luka 1:26).

"Malaika wa Bwana akawajia na utukufu ukawaangazia pande zote … mara likatokea jeshi kubwa la malaika wa mbinguni wakimtukuza Mungu na kusema, Utukufu kwa Mungu juu, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia" (Luka 2:9-14).

"Wao (malaika) sio roho watumikao wakitumwa kuwahudumia wale watakarithi wokovu?" (Ebr.1:14).

14) Malaika wanaumbo la namna gani?

Wana miili ya kiroho isiyopatikana na mauti, lakini kwa umbo na sura wafanana na watu.

"Awafanya malaika zake kuwa roho" (Zaburi 104:4)

"Wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua" (Ebr. 13:2).

"Malaika wa Bwana akatokea … Manoa akasema, Wewe ni mtu? … Kwa maana Manoa hujua kwamba malaika alikuwa wa Bwana …" (Waamuzi 13:3,11,16,20,21).

"Malaika wa Bwana alishuka toka mbinguni … amevaa vazi refu jeupe" (Mathayo 28:2; Marko 16:5).

"Malaika alimtokea Cornelio (mdo.10:3) alielezea kuwa mtu alisimama mbele ana mavazi ya kung'aa" (mst wa 30).

Maelezo yanaweza kutolewa kwa ukweli kwamba kwa kuwa malaika wanazungumza maneno ya Mungu na kutimiza amri zake mara nyingi wametajwa katika Biblia kana kwamba ni Mungu.

"Tazama, mimi namtuma malaika aende mbele zako … Jina langu limo ndani yake" (Kutoka 23:20-21). Alinena maneno ya Mungu kwa Israeli.



## NJIA YA WOKOVU

*(Finding Deliverance)*

149) Inawezekana kwa sisi kuokolewa mbali ya kazi aliyoifanya Kristo?

Hapana; Mungu hajatoa njia nyingine yo yote ya wokovu wa mwanadamu kuliko ya Yesu Kristo.

"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" (Matendo 4:12).

"Mimi ni njia ya kweli na uzima; hakuna mtu ajaye kwa Baba, ila kwa njia ya mimi" (Yohana 14:6).

"Kama msiposadiki kuwa mimi ndiye, mtakufa katika dhambi zenu" (Yohana 8:24).

"Zamani zile mlikuwa hamna Kristo, mmefarakana na jamii ya Israeli, wageni wasio na maagano ya ahadi ile, mlikuwa hamna tumaini, hamna Mungu duniani" (Waefeso 2:12).

150) Ni kwa njia gani tunaletwa katika muungano na kazi ya wokovu iliyotimizwa ndani ya Kristo?

Kwa kuamini ahadi za Mungu kwa kuungana na Kristo kwa ubatizo.

"Pasipo kuamini hatawezekana kumpendeza Mungu" (Waebrania 11:6).
"Ninyi nyote ni wana wa Mungu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu" (Wagalatia 3:26).

"Atakaye amini na kubatitwa ataokoka" (Marko 16:16).

"Kama wengi mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo … na kama ninyi ni wa Kristo basi … warithi sawasawa na ahadi" (Gal.3:29).

## IMANI

*(Faith)*

151) Imani ni nini?

Imani ni tendo linalo toka moyoni na kutufanya tuamini au tusadiki kwa ahadi za Mungu alizozifanya. Imani inatokana na kusoma neno la Mungu na kuelewa mafunzo yake.

147) Basi, mauti kamwe haita ondolewa?

Kifo kitaondolewa kwa utawala wa Kristo. Mwisho wa miaka 1000 ya utawala wa Kristo, utakuwepo ufufuo wa mwisho na hukumu hapo waaminifu kati ya watu watapewa kutokufa na wasio waaminifu watahukumiwa kwa mauti ya pili. Wakati huo mauti itakomeshwa, naye Kristo atampa Baba Ufalme, ili Mungu awe yote kwa watu wote.

"Adui wa mwisho kuondolewa ni kifo" (1 Wakorintho 15:26).

"Kifo hakita kuwepo tena, wala huzuni, au sauti ya kulia" (Ufu. 21:4).

"Ndipo mwisho utafika, wakati atakapompa Mungu Baba huo Ufalme; atakapoweka chini utawala wote na mamlaka na nguvu; maana imepasa sharti amiliki yeye kwanza mpaka awaweke maadui zake wote chini ya nyayo zake" (1 Wakorintho 15:24-25).

148) Mauti yatakapo ondolewa duniani, Je! dunia itaharibiwa?

Hapana; dunia itadumu milele, itajaa utukufu wa Mungu na watu Wake wenye furaha wasiokufa.

"Wala hapatakuwa na laana yoyote tena: bali kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana Kondoo kitakuwa ndani yake, na watumwa wake watamtumikia … Kwa kuwa Bwana Mungu awatia nuru, nao watatawala hata milele na milele" (Ufunuo 22:3-5).

"Kwa maana dunia itajazwa maarifa ya utukufu wa Bwana, kama maji yafunikavyo bahari" (Habakuki 2:14).

"Dunia ameiweka imara milele" (Zaburi 78:69).

"Nitakupa (Kristo) miisho ya dunia kuwa milki yako" (Zaburi 2:8).

"Wenye upole watairithi nchi, na kujifurahisha kwa wingi wa amani … na urithi wao utakuwa wa milele" (Zaburi 37:11-18).

"Ufalme wa dunia hii umekuwa ni ufalme wa Bwana wetu na Kristo wake, naye atamiliki milele na milele" (Ufunuo 11:15).



15) Taja nyakati zilizo katika Biblia za malaika walipowatokea watu?

Mara tatu walimtokea Abrahamu; wawili walifika Sodoma; mmoja alishindana na Yakobo, ambaye pia jeshi lilimtokea; mmoja aliwaongoza Israeli kutoka Misri; mmoja alimpinga Balaamu; mmoja alimtokea Gidioni; mmoja kwa Manoa; mmoja kwa Daudi; mmoja kwa Danieli; mmoja aliliangamiza jeshi la Senakaribu; mmoja alimtokea baba wa Yohana Mbatizaji; mmoja kwa mama yake Yesu; mmoja kwa wachungaji; mkutano uliimba katika bonde la Bethelehemu. Wakati wa ufufuo wa Kristo pia walitokea na kwa nyakati mbalimbali walitokea kwa Mitume baada ya kupaa kwake Kristo.

Mw. 18:1; Mw. 19:1; Mw. 32:24 kwa muungano na Hosea 12:4; Mw. 32:1; na Kut. 14:19-24; Hesabu 22:22; Waamuzi 6:11; 13:3-16; 2 Samueli 24:16; Dan. 9:21; 10:7-12; 2 Wafalme 19:35; Luka 1:11-26; 2:9; Mathayo 28:2; Luka 24:4; Matendo 1:10; 5:19; 12:7-11; Ufunuo 1:1; 22:16.

## MTU *(Man)*

16) Biblia yatufundisha nini kuhusu chanzo cha mtu?

Mtu wa kwanza aliumbwa na Mungu kutoka mavumbi ya ardhini, akatiwa nguvu kwa pumzi ya uhai, naye akawa "nafsi hai" au kiumbe kinachoishi. Mtu wa kwanza aliumbwa kwa "mfano wa Mungu".

"Bwana Mungu akamfanya mtu wa kutoka mavumbi ya ardhi, akampulizia Pumzi puani, mtu akawa nafsi hai" (Mw. 2:7)

"Mungu akaumba mtu kwa mfano wake" (Mw. 1:27).

17) Je! Mtu amegeuka na kukua toka viumbe wa chini?

Biblia haijui lolote kuhusiana na kugeuka (kubadlika). Mtu ni uumbaji maalum, tofauti na wanyama wa ulimwengu, amevikwa sifa ya taji ya kazi ya uumbaji wa Mungu.

18) Je! Mtu hapatikani na mauti, tangu alipoumbwa kwa mfano wa Mungu?

Hapana: Biblia yatuambia kwamba Mungu pekee ndiye hapatikani na mauti: mtu ni mfu – anatawaliwa na mauti.

Mungu "peke yake hapatikani na mauti, amekaa katika nuru isiyoweza mtu kuikaribia, wala hakuna yeyote aliyemwona, wala anayeweza kumwona" (1 Tim.6:16).
"Mtu anayekufa anaweza kuwa na haki kuliko Mungu" (Ayubu 4:17).
"Wewe ni mavumbi na mavumbini utarudi" (Mw. 3:19).
"Ni mwanaume gani atakayeishi asipatikane na mauti? Je! Ataiokoa nafsi yake na mkono wa kaburi?" (Zaburi 89:48).

19) Ni kweli kwamba nafsi (roho) ya mtu haifi?

Hapana. Fundisho hili halijulikani kabisa katika Maandiko. Ingawa Biblia inataja neno roho (nafsi) mara mia kadhaa, kamwe haitaji roho isiyo kufa bali mara nyingi inasema kuwa nafsi hufa.

"Roho inayotenda dhambi, itakufa" (Ezekieli 18:4,20).

"Ni mwanaume yupi atakaye ishi asiione mauti? Atiokoa roho yake na mkono wa kuzimu?" (Zaburi 89:48).

"Hakuziepusha roho zao na mauti, bali aliiachia tauni uhai wao" (Zab. 78:50).

20) Je! Mautini upo uhai wowote basi?

Mtu anapokuwa mautini hawi na fahamu za aina yoyote. Amekufa, hajui lolote ni kwamba kama hakuwahi kuzaliwa.

"Waliohai wanajua kuwa watakufa, bali wafu hawajui chochote" (Mhu. 9:5).

"Mautini hapana kumbukumbu lako" (Zab. 6:5).

"Hapa kazi, wala shauri, wala maarifa, wala hekima kaburini uendako" (Mhubiri 9:10).

"Pumzi yamtoka, anarudi mavumbini, na siku hiyo hiyo mawazo yake yapotea" (Zaburi 146:3-4).

"Kaburi haliwezi kukusifu; mauti haiwezi kukuadhimisha: washukao katika shimo hawawezi kuitarajia kweli yako. Aliye hai, naam, aliye hai ndiye atakusifu kama mimi leo" (Isaya 38:18-19).

21) Kwa nini mtu yupo sasa katika hali mbaya ya kufa?

Mtu ni mfu kwa sababu ya dhambi. Ni sheria ya Mungu ya kuwa watenda dhambi inabidi wafe. Adamu, baba yetu wa kwanza, alitenda dhambi, naye akahukumiwa kufa. Mauti yalianza naye, nayo yametufikia sisi kwa njia yake. Tumerithi umbile alilokuwa nalo baada ya kuwa ametenda dhambi na kuhukumiwa kufa. Tena, sisi sote ni wenye dhambi, na kwa sababu hii tupo chini ya adhabu ya kufa.

"Mshahara wa dhambi ni kufa" (Rumi 6:23).

"Kwakuwa umekula mti niliokuagiza usile … umavumbi wewe na mavumbini utarudi" (Mw. 3:17-19).



145) Je! mataifa mengine ya ulimwengu yatashiriki mibaraka ya Ufalme wa Mungu uaokuja duniani?

Bila wasiwasi; ingawa Israeli atakuwa wa kwanza kati ya mataifa, watu wote wataufurahia utawala wake Yesu. Mungu ataheshimiwa, haki itawekwa na amani ya uhakika, dhambi zitazuiwa, na wanadamu wote watabarikiwa.

"Dunia itajawa na maarifa ya Bwana kama maji yaifunikavyo bahari" (Isa. 11:9).

"Tazama, mfalme atatawala kwa haki, na wakuu watatawala kwa hukumu; na mwanadamu atakuwa kama mahali pa kujificha na upepo na mahali pa kujisitiri na dhoruba; kama mito ya maji mahali pa kavu, kama kivuli cha mwamba mkubwa katika nchi yenye uchovu. (Isaya 32:1,2).

"Naye atafanya hukumu kati ya mataifa mengi, atawakemea watu wa kabila nyingi; nao watafua panga zao ziwe majembe, na mikuki yao iwe miundu: taifa halitainua upanga juu ya taifa lingine, wala hawatajifunza vita tena kamwe" (Isaya 2:4).

"Atawahukumu walioonewa na watu, atawaokoa wahitaji, na kumseta mwenye kuonea … Jina lake litadamu milele: litaendelea jina lake kama jua: mataifa yote yatajibariki katika yeye: nayo yatamwita mbarikiwa" (Zaburi 72:4,17).

"Mataifa yatajibariki katika yeye, nao watajitukuza katika yeye" (Yeremia 4:2).

"Katika siku hiyo litasimama shina la Yese kuwa ishara kwa kabila za watu, yeye ndiye mataifa watamtafuta; na mahali pake pa kupumzika patakuwa na utukufu" (Isaya 11:9,10).

146) Je! mataifa, ukijumuisha taifa la Israeli, yatakuwa na watu wanmaokufa au wasiokufa wakati wa utawala wa Kristo?

Watakuwa wanakufa. Yesu pekee na washirika wake wa kutawala, watakatifu, ndio watakuwa hawafi. Bado mauti itakuwepo, lakini maisha ya wanadamu yatarefushwa sana, nao watu wanaoishi wakati huo watakuwa huru kutokana na udhaifu mwingi ambao unawatesa kwa sasa.

"Hatakuwepo tena mtoto wa siku chache, wala mzee asiyetimiza siku zake; kwa maana mtoto atakufa mwenye umri wa miaka mia, bali mtenda dhambi mwenye umri wa miaka mia atalaaniwa … maana kama siku za mti ndivyo zitakavyokuwa siku za watu wangu, na wateule wangu wataifurahia kazi ya mikono yao muda wa siku nyingi!" (Isaya 65:20-22).

"Tazama mtu huyu ambaye jina lake ni Chipukizi; naye atakuwa katika mahali pake, naye atalijenga hekalu la Bwana. Naam, yeye atalijenga hekalu la Bwana; naye atauchukuwa huo utukufu; ataketi akimiliki kiti chake cha enzi; naye atakuwa kuhani katika kiti chake cha enzi, na shauri la amani litakuwa kati ya hao wawili" (Zekaria 6:12,13).

143) Yesu alipokuja miaka 1,900 iliyopita Wayuda walimkataa kuwa Mfalme wao. Je! watamkubali atakapo kuja tena?

Ndiyo. Yesu atawakomboa kutoka katika mikono ya maadui zao, nao watamtambua kuwa ndiye ambaye baba zao walimsulubisha. Wakiwa na toba ya kutoka moyoni kwa ujinga wa taifa leo, watampokea kwa furaha kama Mwokozi wao.

"Watamtazama yeye waliyemchoma" (Yohana 19:37).

"Nitawamwagia nyumba ya Daudi na wenyeji wa Yerusalemu roho ya kuomba na neema, nao watamuombolezea … nao wataona unchungu kwa ajili yake kama mtu anavyomuonea uchungu mzaliwa wa kwanza wake" (Zekaria 12:10).

"Tazama nyumba yenu imeachwa ukiwa: nami nawaambia hamtaniona tena kamwe, hata mtakaposema, Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana" (Luka 13:35).

144) Israeli utakapokuwa Ufalme, Je! watakuwa chini ya agano na Mungu alilofanya nao waliopokuwa pamoja na Musa kwenye mlima Sinai?

Hapana. Mungu atafanya agano jipya nao, ambalo litafanya dhambi zao wasamehewe.

"Nitafanya agano jipya na nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda. Si kwa mfano wa agano nililofanya na baba zao, katika siku ile nilipowashika mkono ili kuwatoa katika nchi ya Misri; ambalo agano langu hili walilivunja, ingawa nalikuwa mume kwao, asema Bwana. Bali agano hili ndilo nitakalofanya na nyumba ya Israeli, baada ya siku zile, asema Bwana; Nitatia sheria yangu ndani yao, na katika mioyo yao nitaiandika; nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. Wala hawatamfundisha kila mtu jirani yake, na kila mtu ndugu yake, wakisema, Mjue Bwana; kwa maana watanijua wote, tangu mtu aliye mdogo miongoni mwa hao aliye mkubwa asema Bwana; dhambi yao sitaikumbuka tena" (Yeremia 31:31-34).

"Watu wako nao watakuwa wenye haki wote: watairithi nchi milele: Chipukizi nilillolipanda mimi mwenyewe, kazi ya mikono yangu mwenyewe, ili nitukuzwe" (Isaya 60:21).



"Kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na mauti kwa dhambi; mauti yamewafikia wote" (Rumi 5:12).

"Katika Adamu wote wanakufa" (1 Kor. 15:22).

"Kwa kosa la mtu mmoja, hukumu imewafikia watu wote" (Rumi 5:18).

"Wote wametenda dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" (Rumi 3:23).

22) Je! Mungu amekusudia wanadamu wawe daima katika hali hii mbaya ya kufa?

Hapana: Amedhamiria kuondoa dhambi yote duniani, na kukomesha mauti.

"Nitawakomboa toka nguvu za mauti; nitawaokoa na nguvu za kaburi. Ewe mauti yapowapi mapigo yako; Ewe kaburi nitakuangamiza" (Hosea 13:14).

"Atameza mauti kwa kushinda" (Isaya 25:8).

"Hakutakuwa na kifo tena, wala sauti ya huzuni na kulia" (Ufunuo 21:4).

"Adui wa mwisho kuharibiwa ni mauti" (1 Kor. 15:26).

23) Ni kwa njia gani Mungu ataleta matokeo yenye fadhili hii?

Kwa njia ya kipawa cha Mwanawe mpendwa – Bwana Yesu Kristo – aliyemtuma kwa kazi kubwa ya kuziondoa dhambi, na kufungua njia ya uzima wa milele.

"Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanae wa pekee ili kila aaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16).

"Mshahara wa dhambi ni mauti, bali zawadi ya Mungu ni uzima wa milele kwa njia ya Yesu Kristo Bwana wetu" (Rumi 6:23).

"Tazama, Mwana Kondoo wa Mungu aichukuae dhambi …" (Yohana 1:29).

"Yesu aliziondoa dhambi kwa dhabihu ya nafsi yake" (Ebr. 9:26).

"Amebatilisha mauti, ameleta uzima na kutokuharibika kwa ile injili" (2 Tim. 1:10).

24) Dhambi ni nini?

Dhambi ni uasi kwa sheria za Mungu.

"Kila atendaye dhambi, afanya uasi; kwa kuwa dhambi ni uasi" (1 Yohana 3:4).

25) Shetani anayetajwa katika Biblia ni nani?

Kwa neno Shetani kwa lugha ya Kiebrania maana yake ni adui, na linaeleza mmoja akipingana na mwingine. Malaika alikuwa adui kwa Balaamu, na Petro kwa Yesu. Neno hili limefasiriwa "kupinga" au kuwa adui katika Biblia za kutoa ufafanuzi pembezoni, kwa swala la Balaamu. Hili neno limetumika na zaidi kutaja yote yaliyo kinyume na mapenzi ya Mungu na hivyo maana yake ni mwelekeo wa tabia mbovu katika mioyo ya watu.

"Malaika wa Bwana akamwambia, Kwanini umempiga punda wako mara hizi tatu? Tazama, mimi nimekuja ili kukupinga kwa kuwa njia zako zimepotoka mbele zangu" (Hesabu 22:32).

"Yesu akageuka na kumwambia Petro. Rudi nyuma yangu wewe, Shetani; maana ukikwazo kwangu" (Mathayo 16:23).

"Kwa hiyo tulitaka kuja kwenu, naam, mimi Paulo, mara ya kwanza na mara ya pili; lakini Shetani akatuzuia" (1 Wathesalonike 2:18).

"Petro akamwambia Anania, kwa nini Shetani ameujaza moyo wako hata ukasema uongo wa kumdanganya Roho Mtakatifu, na kufucha thamani ya kiwanja?" (Matendo 5:3).

26) Na Ibilisi wa Biblia naye ni nani?

Neno hili linamaana msingiziaji nalo linataja mmoja ambaye kwa uongo anasingizia au kudanganya mwingine. Linaweza neno hili kutumika kwa mtu, watawala, au taifa; na hasa linatumika kutaja nguvu ya uovu ndani ya umbile tulilo nalo ambalo huchongea kwa Mungu kwa kudanganya watu kwa kudokeza kwamba Mungu hana maana ya anayosema. Yesu alishinda kila kishawishi kilichotaka kumvuta atende dhambi na mwisho ataondoa maovu yote yanayo sababishwa na dhambi toka duniani.

"Yesu akawajibu akasema, sijawachagua ninyi kumi na mbili, na mmoja wenu ni ibilisi? Alimtaja Yuda Isikarioti, mwana wa Simoni: maana yeye ndiye atakaye msaliti, kwa kuwa alikuwa mmoja wa wale thenashara". (Yohana 6:70,71).

"Ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani mjaribiwe; nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi" (Ufunuo 2:10).

"Yesu mwenyewe alishiriki yale yale (mwili na damu); ili kwa njia ya mauti aweze kumharibu yeye aliye na nguvu za mauti yaani Ibilisi" (Ebrania 2:14).

"Atendaye dhambi ni wa ibilisi: maana ibilisi anatenda dhambi tangu mwanzo. Kwa makusudi haya Mwana wa Mungu alidhihirika ili amharibu ibilisi na kazi zake" (1 Yohana 3:8).



"Tazama siku zinakuja, asema Bwana, nitakapolitimiza neno lile jema nililolinena, katika habari za nyumba za Israeli na Yuda. Katika siku zile, na wakati ule, nitamchipushia Daudi Chipukizi la haki; naye atafanya hukumu na haki katika nchi hii. Katika siku zile Yuda ataokolewa na Yerusalemu utakaa salama, na jina lake atakaloitwa ni hili, "Bwana ni haki Yetu" (Yeremia 33:14-16).

141) Ufalme wa Mungu unaokuja duniani utakuwa na mji gani mkuu?

Yerusalemu: "mjiwa Daudi" wa zamani, utakuwa umerudishwa na kuboreshwa, na kuwa mji kwa wakati huo mkuu wa dunia.

"Wakati huo watauita Yerusalmemu kiti cha enzi cha Bwana; na mataifa yote watakusanyika huko Yerusalemu, kwa ajili ya Jina la Bwana: wala hawatakwenda tena kwa ukaidi wa moyo wao" (Yeremia 3:17).

"Nao watakuita mji wa Bwana, Sayuni wa Mtakatifu wa Israeli" (Isa. 60:14).

"Na Bwana atawamiliki katika mlima Sayuni … Ufalme utakuja kwa binti wa Yerusalemu" (Mika 4:7,8).

142) Ni nani atakuwa Mfalme wa Ufalme wa Mungu uliorudishwa?

Bwana Yesu Kristo, wa uzao wa Daudi, Mwana wa Mungu, atakayerudi kutoka mbinguni na kuja kufanya kazi kubwa ya kusimamisha Ufalme wa Mungu hapa duniani.

"Utamwita jina Yesu. Atakuwa mkuu, naye ataitwa Mwana wa Aliye juu: na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha baba yake Daudi. Atamiliki nyumba ya Yakobo milele; nao ufalme wake hautakuwa na mwisho" (Luka 1:30-33).

"Yesu akawaambia, Amini, nawaambia ya kwamba ninyi mlionifuata mimi, katika ulimwengu mpya, atakapoketi Mwana wa Adamu, katika kiti cha utukufu wake, nanyi mtaketi katika viti kumi na viwili, mkiwahukumu kabila kumi na mbili za Israeli" (Mathayo 19:28).

"Kwa nyongeza ya enzi yake na amani haitakuwa na mwisho kamwe, juu ya kiti cha enzi cha Daudi na mfalme wake; kuthibitisha na kutegemeza kwa hukumu na haki, tangu sasa na hata milele. Wivu wa Bwana wa majeshi ndio utakaotenda hayo" (Isaya 9:7).

"Katika siku zile, na wakati ule, nitamchipushia Daudi Chipukizi la haki; naye atafanya hukumu na haki katika nchi" (Yeremia 33:15).

135) Ni manabii gani aliowainua Mungu katika Yuda wakati wa kipindi hiki cha matengezezo?

Hagai, Zekaria na Malaki.

136) Ni nani aliandika, kwa uongozi wa Mungu, kitabu cha mwisho cha Agano la Kale?

Malaki.

137) Kazi hii ilikuwa miaka mingapi kabla ya kuzaliwa Yesu Kristo?

Karibu miaka 400.

138) Je! hapakuwa na neno la Bwana wakati huu wa kipindi kirefu kutoka Malaki hadi kwa Yohana Mbatizaji? Jambo hili Biblia yaeleza vipi?

"Njaa ya kusikia maneno ya Mungu" (Amosi 8:11,12).

**KUKUSANYIKA TENA ISRAELI NA KUJA KWA UFALME WA MUNGU**
*(The Gathering of Israel into The Kingdom of God)*

139) Ufalme wa Israeli na Yuda akiisha kuupindua Mungu, na watu wao kutawanywa kati ya mataifa, Je wataungana tena?

Ndiyo. Mungu amesema kwamba atawakusanya tena na kuwapanda wawe taifa moja katika nchi yao wenyewe.

"Sasa nitawarejeza watu wa Yakobo waliohamishwa, nitawahurumia nyumba yote ya Israeli" (Ezekjieli 39:21-25).

"Aliyemtawanya Israeli atamkusanya tena, na kumlinda kama mchungaji alindavyo kundi lake" (Yeremia 31:10)

"Atawakusanya Israeli waliotupwa, na kuwakusanya pamoja Yuda waliyo tawanyika kutoka pande nne za dunia" (Isaya 11:12).

140) Ufalme wa Israeli wakati huo utarudishwa?

Ndiyo; Mungu amesema. Ufalme huo utakuwa ni kitovu cha huo ujao duniani.

"Nitawatwa wana wa Israeli toka kati ya mataifa walikokwenda, nami nitawakusanya pande zote, na kuwaleta katika nchi yao wenyewe: nao watakuwa taifa moja juu ya milima ya Israeli; na mfalme mmoja ndiye atakuwa Mfalme wao wote" (Ezekieli 37:21,22).



Hii inatuleta katika tafakari ya mafundisho ya Biblia juu ya:-

**YESU KRISTO** *(Jesus Christ)*

27) Yesu Kristo alikuwa ni nani?

Yesu Kristo alikuwa ni Mwana wa Mungu.

"Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye nimependezwa naye" (Matthayo 3:17).

"Mimi ni Mwana wa Mungu" (Yohana 10:36).

"Wewe ni Mwana wa Mungu" (Yohana 1:49).

"Nimeona, nami namshudia ya kuwa huyu ni Mwana wa Mungu" (Yohana 1:34).

28) Je! Yesu Kristo alikuwa ni mwanadamu, ingawa alikuwa ni Mwana wa Mungu?

Ndiyo, alikuwa ni mtu, kwa mambo yote kama sisi wenyewe, lakini katika sifa ya tabia alikuwa hana dhambi.

"Yesu wa Nazareti, mtu aliyethihirishwa kwenu na Mungu kwa miujiza na ajabu na ishara, ambazo Mungu alizifanya kwa mkono wake …" (Mdo. 2:22)

"Yupo mmoja mpatanishi kati ya Mungu na watu, mwanadamu Kristo Yesu" (1 Tim. 2:5).

"Kwa njia ya mtu huyu mnahubiriwa msamaha wa dhambi" (Mdo. 3:38).

"Kwa mambo yote ilimpasa afanane na ndugu zake" (Ebr. 2:17).

"Alijaribiwa katika njia zote kama sisi, lakini hakutenda dhambi" (Ebr. 4:15).

29) Ni kwa njia ipi Yesu Kristo alikuwa na yote mawili mtu halafu Mwana wa Mungu?

Kwa sababu Mungu alikuwa ni Baba yake; kwa hivi alikuwa ni Mwana wa Mungu. Mariamu, bikira alikuwa ni wa ukoo wa Daudi, alikuwa ni mama yake; kwa sababuhiyo "alikuwa ni Mwana wa Daudi", na akisha kuwa hivi mtu akawa mshirika wa mwili wetu wa asili. Yesu anasema yeye mwenyewe kuwa ni Mwana wa Mungu na pia Mwana wa Adamu (Yohana 5:25,27).

"Roho Mtakatifu atakujia, uweza wa Aliye juu zitakufunika: kwa hiyo kitu kitakacho zaliwa toka kwako ataitwa Mwana wa Mungu" (Luka 1:35).

"Yesu Kristo, mwana wa Daudi, mwana wa Abrahamu" (Mathayo 1:1).

"Mungu alimtuma Mwanae aliyezaliwa na mwanamke" (Wagalatia 4:4).

"Alionekana ni mwanadamu" (Wafilipi 2:8).

"Aliguswa na udhaifu tulio nao, kwa mambo yote alijaribiwa kama sisi bali hakutenda dhambi" (Ebr. 4:15).

30) Je! Yesu alikuwa na mambo mawili uungu na ubinadamu basi wakati huo?

Alikuwa ni mwanadamu kwa kuwa alikuwa ni mwana wa Mariamu; lakini wa Mungu sababu alizaliwa kwa nguvu zake Mungu ya Roho Mtakatifu: toka kwa Roho huyo alipata hekima; mfano mzuri wa tabia aliyokuwa nayo. Kwa hivi Yesu alimdhihirisha Mungu katika mwili wa mwanadamu.

"Nimeshuka kutoka mbinguni" (Yohana 6:38).

"Hapo mwanzo kulikuwako neno … naye neno alikuwa Mungu … Nalo neno likafanyika mwili, na kukaa pamoja nasi (nasi tuliuona utukufu wake, utukufu wa mwana mpendwa pekee wa Baba" (Yohana 1:1,14).

"Kwa kuwa watoto wanashiriki damu na mwili, naye(Yesu) alishiriki yayo hayo" (Ebr.2:14).

"Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake" (2 Wakorintho 5:19).

"Aliyeniona mimi amemwona Baba" (Yohana 14:9).

**JINA LA YESU KRISTO** *(The Name of Jesus Christ)*

31) Ni kwanini Yesu Kristo aliitwa kwa jina hilo?

Ili kuonyesha kuwa yeye ni nani na kazi yake ni ipi. Yesu ni jina la – Kiebrania kwa asili, likimaanisha **Mungu ataokoa**: Kristo ni neno la Kiyunani (Kigriki), maana yake ni **mpakwa mafuta**, likiwa linaonyesha kwamba ameteuliwa na Mungu ili kuwa mfalme. Kupakwa mafuta ni tendo ambalo zamani wafalme na makuhani walikuwa wanafanyiwa uteuzi kwa mtu akiwa ametumwa na Mungu kuwekwa katika kazi zao. Sherehe huwana mchanganyiko wa kuwamiminia mafuta matakatifu juu ya vichwa. Lakini Yesu mafuta aliyopakwa yalikuwa ni tofauti, kwani haya ya zamani ni mfano. Yeye alipakwa mafuta na Roho wa Mungu wakati wa ubatizo wake mtoni Yordani. Jina Yesu Kristo, kwa sababu hii, maana yake ni kuwa Mwokozi aliye Mfalme.



123) Ufalme wa Israeli ulitawaliwa na wfalme wangapi? Kati ya hao ni wangapi walikuwa ni wafalme wazuri? Ni alama gani maalum unazozikumbuka kuhusu Ahabu, Yehu?

124) Ni manabii gani wakuu walioishi Israali wakati wa kipindi hiki?

125) Kwa namna ipi Ufalme wa Israeli ulifika mwisho? Ni nani aliutwaa, na ilitokea nini kwa watu wake?

126) Wafalme wangapi walitawala Ufalme wa YUDA? Ni wangapi kati yao walikuwa ni wafalme wazuri? Sema unachokijua kwa Asa, Yehoshafati, Hezekia na Yosia.

127) Nani alikuwa ni Mfalme wa mwisho wa Yuda? Nini kilitokea wakati wa utawala wake?

2 Wafalme 24; Yeremia 52.

128) Ni unabii gani wa muhimu alioutoa Mungu kuhusiana na kiti alichokikalia Daudi?

Ezekieli 21: 25

129) Je! Unabii huo umetimia? Kama sio, jinsi gani na ni lini unabii utatimia?

Luka 1:31-33

130) Yuda walikaa utamwani Babeli kwa muda gani?

Yeremia 25: 8-12; 29:10-14

131) Jinsi gani ahadi ya Mungu kwa habari ya kurudi Wayahudi katika nchi yao ilitimia?

Ezra 1:1; Isaya 44:28.

132) Ni nani walikuwa wakuu wa Wayahudi ambao walirudi kutoka Uhamishoni ili kujenga tena Hekalu la Bwana kwenye mji wa Yerusalemu?

Kwanza, Zerubbabeli na Yoshua; halafu Ezra na Nehemia.

133) Katika kipindi hiki Ufalme wa Daudi ulirudi?
Hapana. Kulikuwa hakuna mfalme Yerusalemu; mji ulikuwa chini ya mamlaka ya Uajemi.

134) Eleza kwa kifupi kwa kile Zerubbabeli, Ezra na Nehemia walichomaliza kwa kazi yao katika mji wa Yerusalemu.

116) Atatambuaje basi utimilifu wa ahadi hizi huyu Daudi?

Atafufuliwa toka wafu Yesu atakaporudi kutoka mbinguni wakati Ufalme wa Mungu utakapo simamishwa.

117) Mara nyingine imesemwa kwamba utawala wa Sulemani ulikuwa ndiyo utimlifu wa agano la Mungu kwa Daudi. Je! ni kweli?

Hapana. Ingawa Sulemani alikuwa ni mwana wa Daudi, naye alimjengea Mungu nyumba, mambo ya muhimu ya kuangaliwa ya agano la Mungu hayakutambulika katika kipindi cha utawala wake. Kiti cha enzi cha Sulemani hakikuimarishwa imara milele; alimkosea Mungu kwa kufuata sanamu na miaka iliyofuata baadaye utawala wake ulionekana kuwa na dhuluma na uchungu.

118) Onyesha ni kwa maneno yapi Yesu Kristo anatimiza ahadi ya Mungu kwa habari ya "mzao" wa Daudi.

Mungu alikuwa ni Baba yake; alikuwa an Mwana wa pekee wa Mungu. Ataketi kwenye kiti cha enzi cha Daudi akiwa ni mrithi wa Daudi. Ufalme wake hautakuwa na mwisho. Yeye mwenyewe amesema kuwa ni shina la "mzao wa Daudi".

Luka 1: 30-33; Ufunuo 22: 16.

**UFALME ULIOGAWANYIKA**

*(The Kings)*

119) Ni nani alimfuata Daudi kuwa mfalme? Eleza kwa kifupi matukio makubwa katika utawala wake. Mungu alisemaje kuhusu ufalme wa Sulemani baadaye?

1 Wafalme 11:4-13.

120) Eleza kwa kifupi kuhusu uasi wa kabila kumi katika utawala wa Rehoboamu. Ni nani aliongoza uasi naye akawa ni mfalme wa kabila zilizo jitenga?

1 Wafalme 12.

121) Jinsi gani Yeroboamu alitafuta kudumisha kabila kumi zisiirudie nyumba ya Daudi?

1 Wafalme 12: 27-33

122) Falme mbili, Israeli na Yuda, Je! ziliwahi kuungana tena?



"Utamwita jina lake Yesu: maana ndiye atakaye waokoa watu wake na dhambi zao" (Mathayo 1:21).

"Mungu amemtia mafuta Yesu wa Nazareti kwa Roho Mtakatifu, na nguvu; naye akazunguka huko na huko akitenda kazi njema" (Mdo.10:38).

"Watu wote waliopobatizwa, naye Yesu akabatizwa, na alipokuwa akiomba, mbingu zilifunguka na Roho Mtakatifu alishuka kwa umbo la njiw a juu yake" (Luka 3:21,22).

**KIFO CHA KRISTO** *(Christ's Death)*

32) Ni jinsi gani Mungu anawaokoa watu toka dhambi zao kwa njia ya Kristo?

Ni jambo la Mungu la awali ya kuwa "pasipo kuwapo kumwagika damu basi hakuna ondoleleo la dhambi". Dhabihu zilizo tolewa kwa kufuatana Musa sheria yake ni wazi zilikuwa zinaonyesha jambo hili la awali, ilikuwa ni utabiri wa dhabihu iliyo kamili aliyoitoa Yesu msalabani, damu yake ilipomwagika. Upendo wa Mungu umeonekana kwa kumtoa Yesu kwa kufa awe sadaka kwa ajili ya dhambi, watu wanaweza kusamehewa makosa yote na kumrudia Mungu.

"Tazama, Mwana Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu" (Yohana 1:29).

"Mungu kwa njia ya Kristo amewasamehe" (Efeso 4:32).

"Kwa yeye tunao ukombozi kwa damu yake, naam, msamaha wa dhambi" (Wakolosai 1:14).

"Dhambi zenu mmesamehewa kwa jina lake" (1 Yohana 2:12).

"Mungu akiisha kumfufua Mwana wake Yesu, alimtuma kuwabariki na kuwageuza kila mmoja wenu na dhambi zake""(Mdo.3:26).

"Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake" (2 Wakorintho 5:19).

33) Dhabihu ya Kristo imetimiza vizuri kwa kitu gani basi?

Dhambi imehukumiwa kwa kifo chake msalabani, na haki ya Mungu imejulikana na kushuhudiwa kwa ulimwengu wote kwa kumwagika damu yake. Dhambi zaweza kusamehewa kwa kuwa amefanikisha jambo hili, na njia ya kuelekea uzima wa milele imefunguliwa kwa ufufuo wa Yesu toka wafu. Kwa kuwa utii alikuwa nao kwa mambo yote aliyoagizwa na Mungu, hata kifo kwa njia ya msalaba, Mungu akamfufua toka wafu asife tena. Hivyo amekuwa ni mzaliwa wa kwanza wa uumbaji mpya.

"Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu (Mungu ametimiza) kwa kumtuma mwanawe kwa mfano wa mwili ulio wa dhambi, kwa sababu ya dhambi ili azihukumu katika huu mwili" (Rumi 8:3).

"Mungu amemuweka kuwa kipatanisho kwa njia ya imani kwa damu yake, ili aonyeshe haki yake, kwa kuziondoa dhambi zilizo kwisha kufanywa zamani kwa ustahimili wa Mungu; apate kujulisha haki yake wakati huu" (Rumi 3:25-26).

"Alikuwa ni mtii hata katika mauti, naam, mauti ya msalaba" (Wafilipi 2:8).

34) Ni nini kilitokea baada ya Yesu kusulubiwa?

Alishushwa chini toka msalabani na kulazwa kaburini, lililo tengenezwa na Yusufu wa Arimathaya.

Matg.27:50-60; Marko 15:42-47; Luka 23:50-56; Yohana 19:38-42.

35) Alikaa kaburini kwa muda gani?

Siku tatu.

Mathayo 12:40; Marko 8:31; Luka 24:7

36) Katika siku ya tatu kilitokea nini kwa Yesu?

Mungu alimfufua kotoka kwa wafu.
Ona sura za mwisho za kila injili.

37) Kwa sababu gani Mungu alimfufua Yesu toka kwa wafu?

Kwa sababu ya utii wake wote kwa mambo yote, hata kifo cha msalaba. Na kwa kuwa alikuwa ni mwenye haki (mkweli) haikuwezekana mauti mtu huyu imshikilie, ambayo ni mshahara wa dhambi.

"Mungu alimfufua siku ya tatu" (Mdo. 10:40).

"Ambaye Mungu alimfufua, akiufungua uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao" (Mdo. 2:24).

"Alikuwa mtii hata kwa mauti ya msalaba, kwa hiyo Mungu amemwadhimisha mno, na kumpa jina lipitalo majina""(Wafilipi 2:8,9).

38) Jinsi gani ufufuo wa Yesu unatofautiana na wa wale waliofufuliwa zamani kwa mfano Lazaro?



## AGANO LA MUNGU ALILOFANYA NA DAUDI

*(God's Rule through David)*

111) Ni hali gani ya mambo katika maisha ya Daudi yaliyompeleka Mungu kufanya agano naye?

Nia ya Daudi kujenga nyumba inayofaa kwa ajili ya Sanduku la Agano la Mungu.

2 Samueli 7:1-3.

112) Mungu alimjibu nini Daudi?

Badala ya Daudi kumjengea Mungu nyumba, Mungu atamjengea Daudi "njumba", na akaahidi kwamba kiti chake cha enzi kitaimarishwa imara milele mbele ya Daudi, ingawa jambo hili litachukua muda baada ya kifo cha Daudi, hadi "mzao" wake atakapoketi kwenye kiti cha enzi.

2 Samueli 7:11-16; Zaburi 89: 3,4.

113) Je! Mungu alitaja jambo lolote kwa watu wa Israeli katika ahadi hizi kwa Daudi?

Ndiyo. Aliahidi kwamba Israeli watawekwa mahali pao wenyewe, na kamwe hawataondoshwa, na kwamba watakuwa huru kutoka mateso yatokayo kwa maadui zao.

2 Samueli 7:10

114) Ni jambo gani maalum la kuangaliwa kwa habari ya mzao wa Daudi ulioingizwa katika ahadi za Mungu kwa Daudi?

Mungu atakuwa Baba yake, na kwa sababu hiyo anakuwa ni Mwana wa Mungu; atajenga nyumba kwa ajili ya jina la Mungu, na kiti chake cha enzi na ufalme utaimarishawa milele.

2 Samueli 7: 12-14.

115) Je! Daudi alizitegemera hizi ahadi za Mungu kutimilika katika wakati wa uhai wa maisha yake?

Hapana; alitambua kwamba utimilifu wake ni muda mrefu mbele – ng'ambo ya pili ya muda wa maisha yake.

2 Samueli 7:10; 2 Samueli 23:5.
(Jifunze 2 Samueli 23, mstari wa 1-5).

103) Sema unachokijua kwa kila mmoja wa hapo juu.

104) Ni kitabu gani kingine katika Biblia kinachotuambia matukio yaliyotokea katika siku za Waamuzi?

Ruthi 1:1.

105) Ni maneno gani yanayomaliziwa kwa Kitabu cha Waamuzi?

Waamuzi 21:25.
(Mstari mwingine unaostahili kukumbusha)

## ISRAELI INAKUWA UFALME

*(The Kingdom of Israel)*

106) Mwamuzi wa mwisho wa Israeli alikuwa nani?

1 Samueli 7:15.

107) Kwa sababu gani Israeli walitaka mfalme badala ya kuwa chini ya mwamuzi? Kwa ombi lao Samueli aliwajibu nini?

1 Samueli 8:5.

108) Kwa ombi la wa-Israeli Mungu aliwajibu nini?

1 Samueli 8:7.
(Jifunze maneno: "Hawajakukataa wewe (Samueli), bali wamenikataa MIMI, ili nisiwatawale.")

109) Mfalme wa kwanza wa Israeli alikuwa nani? Eleza tabia yake. Kwa sababu gani alikataliwa?

1 Samueli 10:24; 13:13,14; 15:10-26.

110) Mungu alimteua nani kushika nafasi ya Sauli? Mungu aliipimaje tabia ya Sauli?

1 Samueli 16:1-13. Matendo 13:22. 1 Wafalme 15:5.



Hawa walifufuliwa kwa kufanywa upya tu wa maisha haya; lakini Yesu yeye alifufuliwa ili kupata uzima wa milele.

"Kristo akiisha fufuliwa toka wafu hafi tena: mauti haina utawala juu yake" (Rumi 6:9).

"Amepewa nguvu za uzima usio na mwisho" (Ebr. 7:16).

"Mimi nihai, niliyekuwa nimekufa, tazama mimi niko hai milele na hata milele" (Ufunuo 1:18).

39) Kwa maana ipi ufufuo wa Kristo ni wa muhimu kwa wokovu wetu?

Kwa kuwa kifo cha Kristo kilikuwa ni cha muhimu kwa kuondoa dhambi, basi ufufuo wake ni wa muhimu kwa sababu ya kufungua njia ya kutokufa. Mwakozi anayekufa (au mfu) hawezi kuwakomboa watu kutoka katika mauti.

"Ikiwa Kristo hajafufuka imani yenu ni bure, mngalimo katika dhambi" (1 Kor. 15:17)

"Kama katika Adamu wote hufa, kadhalika walio katika Kristo watahuishwa" (1 Kor. 15:22).

"Mshara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu" (Rumi 6:23).

"Na hii ndiyo habari, ya kwamba Mungu ametupa uzima wa milele, na uzima huu umo katika Mwana" (1 Yohana 5:11).

"Kwa sababu mimi ni hai, nanyi pia mtaishi" (Yohana 14:19).

40) Kristo amesemwa kuwa ni "limbuko lao waliolala". Maana yake nini?

Ni wa kwanza kufufuliwa na kupata uzima wa milele; lakini kwa kifo chake na ufufuo wale wanao mwamini, wameunganika naye kwa ubatizo, na wanamfuata kwa uaminifu, watafufuliwa kutoka wafu atakapokuja, na baada ya hukumu watafanywa wasife. "Limbuko" linadokeza uwepowa "mavuno" ya baadaye.

"Sasa Kristo amefufuka amekuwa limbuko lao waliolala … Lakini kila mmoja kwa namna yake: Kristo ni limbuko; baadaye wale walio wa Kristo atakapo kuja" (1 Kor. 20:23).

"Yeye ni kichwa cha mwili, kanisa … mzaliwa wa kwanza toka waliokufa" (Wakolosai 1:18).

## **KUPAA KWA KRISTO** *(The Cleansing of Christ)*

41) Kristo alikaa muda gani duniani baada ya kufufuka? Alishughulika na Jambo lipi?

Siku Arobaini; akiwaambia mitume wake "mambo yaliyohusu ufalme wa Mungu". Matendo ya Mitume 1:2,3

42) Je! Kristo aliwapa agizo lolote Mitume wake kuhusiana na kazi yao baada ya ufufuo wake?

Aliwaagiza waende ulimwenguni pote wahubiri injili kwa kila kiumbe; na kubatiza wale wanao amini; na kuwafunza kushika maagizo ya mambo yote aliyowaamuru.

Mathayo 28:18, 20; Marko 16:16

43) Mitume walitimiza agizo hili?

Ndiyo, rekodi ya shughuli zao tumepewa katika Matendo ya Mitume. Toka Yerusalemu, tunaabiwa kwamba waliihubiri injili na kubatiza katika Uyahudi, Samaria na sehemu zote za ulimwengu wa Kale. Petro na Paulo walikuwa mstari wa mbele kwa kazi hii.

44) Palitokea nini mwishoni mwa siku arobaini za kuwa Yesu na mitume wake baada ya ufufuo wake?

Akapaa kuelekea mbinguni; mitume walimwona akichukuliwa juu. Mitume 1:9; Luka 24:51.

45) Ni nani waliwatokea Mitume muda huu nao walisema nini?

"Watu wawili wakiwa katika mavazi meupe" – malaika wa Mungu, walisema kwa kuwahakikishia mitume ya kuwa Yesu atarudi kama alivyokuwa walipo mwona akielekea mbinguni.

Soma na ujifunze ujumbe wa malaika – Matendo 1:10-11.

## **UKUHANI WA KRISTO** *(Christ's Death)*

46) Ni kazi gani ya muhimu anayoifanya sasa huko mbinguni?

Anatenda kazi ya Upatanishi na ya Ukuhani Mkuu kwa ajili ya ndugu zake walio duniani, akikabidhi maombi yao kwa Mungu, na akimsihi Mungu kwa niaba yao.

"Tunaye kuhani mkuu wa namna hii, aliye keti mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Ukuu mbinguni" (Ebr. 8:1).



93) Kwanini Mungu aliagiza wa-Israeli wawaangamize Wakanaani? Je! Israeli walitimiza jambo hili?

Mambo ya Walawi 18. Kumbukumbu la Torati 20:16-17, 18. Waamuzi 2:1-3.

94) Ni kazi gani ya muhimu ambayo Yoshua aliitimiza baada ya kutwaa Kanaani?

Hesabu 33 – 34. Yoshua 14 – 15.

95) Ni neno gani la mwisho lenye maonyo alilolitoa Yoshua kwa Israeli? Rudia tena tangazo lake:

"Chagueni ni nani hivi leo mtakaye mtumikia … lakini mimi na nyumba yangu. tutamtumikia BWANA" (Yoshua 24:14,15).
(Tangazo hili linastahili kulikumbusha)

## **WAISRAELI WAKIWA CHINI YA WAAMUZI**

*(Israel under the Judges)*

96) Je! Israeli waliendelea kumtumikia BWANA baada ya kifo cha Yoshua? Kwa muda gani walikuwa waaminifu?

Waamuzi 2:7.

97) Ni kwa njia zipi Israeli "walimwacha Bwana"?

Waamuzi 2:1-5. Waamuzi 2:10-13.

98) Ni jinsi gani Mungu aliwaadhibu Israeli kwa dhambi zao?

Waamuzi 2:14-15

99) Mungu alimwinua nani ili kuwaokoa walipotubu?

100) Taja majina baadhi ya Waamuzi ambao Mungu aliwainua.

101) Kipindi cha Waamuzi kilidumu kwa muda gani?

"Kwa karibu muda wa miaka 450" (Matendo 13:20).

102) Ni Waamuzi gani waliotajwa katika orodha ya "wanaostahili" ambao ni wa imani walio orodheshwa kwa Waebrania 11?

(Gideoni, Baraka, Samsoni, Yeftha).

84) Kora, Dathani na Abiramu walikuwa ni akina nani? Walifanya ninin, na kitu gani kiliwapata?

Hesabu 16 – 17.

85) Musa mara mbili aliupiga mwamba kwa fimbo yake. Toa tofauti kwa matukio mawili.

Hesabu 20. Kutoka 16 – 17.

86) Balaamu na Balaki walikuwa ni nani. Eleza kwa kifupi kukutana kwao na matokeo yake.

Hesabu 22 – 24.

87) Kwanini Musa hakuruhusiwa kuingia nchi ya Ahadi? Alikufa wapi? Alikuwa na umri gani?

Hesabu 27:12-23. Kumbukumbu 34.

**KUUTWAA AU USHINDI JUU YA KANAANI**

*(The Conquest into the Land of Canaan)*

88) Mungu alimteua nani ili kushika nafsi ya Musa kuwaongoza Israeli? Alikuwa na sifa gani hata akachukua nafasi ya Musa?

Hesabu 27: 15,23 Yoshua 1 na 2.

89) Toa maelezo ya kuvuka Mto Yordani.

Yoshua 3 na 4

90) Rahabu alikuwa ni nani? Ni kwa njia gani aliwasaidia Israeli?

Yoshua 2.

91) Toa maelezo namna Yeriko ulivyotwaliwa na Israeli? Palitokea nini kwa Rahabu.

Yoshua 6.

92) Akani alikuwa ni nani? Alifanya dhambi gani? Alipata adhabu gani?

Yoshua 7.



"Tunaye kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu Mwana wa Mungu."

"Hatuna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; alijaribiwa katika hali zote kama sisi lakini hakutenda dhambi" (Ebr. 4:14,15).

**KUJA MARA YA PILI KRISTO** *(Christ's Second Coming)*

47) Kwa nini tunauhakika kuwa Yesu Kristo atarudi kutoka mbinguni?

a) Sababu aliwaahidi wafuasi wake kuwa atarudi.

"Naenda kuwaandalia mahali, na nikiisha kuwaandalia mahali kwa ajili yenu, nitarudi tena niwapokee kwangu mwenyewe" (Yohana 14:2,3).

b) Kwa kuwa malaika wa Mungu walisema.

"Huyu Yesu aliyetwaliwa toka kwenu kwenda mbinguni atarudi namna hiyo hiyo mlivyomwona akienda mbinguni" (Mdo. 1:11).

c) Kwa sababu mitume walifundisha jambo hili.

"Mungu atamtuma Yesu Kristo … ambaye ilimpasa apokelewe mbinguni hata vitu vyote vitakapofanywa upya" (Mdo. 3:20,21).

"Bwana mwenyewe atashuka toka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya Malaika mkuu, na parapanda ya Mungu, na wafu katika Kristo watafufuliwa kwanza" (1 Wathesalonike 4:16).

d) Kwa sababu Kristo katika ujumbe wake wa mwisho, toka mkono wa kuume wa Mungu, alinena wazi kuhusu jambo hili.

"Tazama, naje upesi, na ujira upo pamoja nami" (Ufunuo 22:12).

48) Ni kazi gani Yesu atamfanyia Mungu atakaporudi duniani?

Atawafufua watumishi wake waliolala, fanya nao hukumu (uamuzi) na hivyo kuwapa thawabu kulingana na matendo yao; ndipo akiwa na watakatifu hao waliopewa kutokufa watautiisha ulimwengu utii mamlaka ya Mungu. Watu wa Israeli kuwarudisha ambao wametawanyika na kuusimamisha Ufalme wa Mungu duniani.

**UFUFUO, NA KUPASIWA NA HUKUMU** *(The Judgement Seat)*

49) Kristo atafanya nini kwanza atakaporudi?

Atawaita wale wote ambao wanapasiwa na hukumu, wafu au waliohai. Wafu atawafufua; waliohai watakusanywa na malaika wake. Wote yawapasa kusimama mbele ya kiti cha hukumu, ili waweze kupokea kulingana na yaliyofanywa wakiwa katika maisha haya.

"Yesu Kris o atawahukumuwalio hai na wafu atakapotokea" (2 Tim. 4:1).

"Wengi wao waliolala katika mavumbi ya nchi wataamka" (Dan. 12:2).

"Nao watatoka, waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, waliofanya uovu kwa ufufuo wa kuhukumiwa" (Yohana 5:29).

"Yatupasa sisi sot e kusimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mmoja apokee mambo aliyofanya katika mwili iwe ni mema au mabaya" (2 Wakorintho 5:10).

50) Ni nani wanaopasiwa na hukumu?

Wote ambao wanaujua ukweli, iwe wanajiweka katika ukweli au wanaukataa.

"Aiminiye (injili) na kubatizwa ataokolewa: bali asiyeiamini injili atahukumiwa" (Marko 16:16).

"Anayenikana na kutopokea maneno yangu, yupo anayemuhukumu: Neno lile nililosema ndilo litakalo muhukumu siku ya mwisho" (Yohana 12:48).

51) Kuna wengine ambao hawahusiki na hukumu?

Ndiyo, ni wengi. Ni nuru (yaani, kuwa na elimu ya kutosha kwa mapenzi ya Mungu) ndiyo hufanya kuhusika; lakini giza limeifunika dunia; na palipo na giza, dhambi haihesabiki.

"Na hii ndiyo hukumu, kwamba nuru imekuja ulimwenguni, na watu wamependa giza kuliko nuru, kwa sababu matendo yao ni maovu" (Yohana 3:19).

"Pasipokuwa na sheria hakuna kosa" (Rumi 4:15).

"Dhambi haihesabiwi isipokuwapo sheria" (Rumi 5:13).

"Kama nisingalikuja na kusema nao, wasingalikuwa na dhambi: lakini sasa hawana udhuru kwa dhambi zao""(Yohana 15:22).



75) Eleza au toa maelezo ya Pasaka (Passover) halafu na maana yake.

Kutoka 12 - 13.

76) Palitokea nini Bahari ya Shamu?

Kutoka 14.

77) Eleza kwa kifupi matukio ya Sinai?

Kutoka 19 - 20.

78) Sema tena au kariri Amri Kumi.

Kutoka 20: 2-17.
(Ikiwa watoto hawazifahamu vema, utiwe mkazo wa kuwakumbusha).

79) Ni agano lipi ambalo Mungu alifanya na wa-Israeli pale Sinai?

Kutoka 24.

80) Ni jinsi gani agano la Sinai linatofautiana na agano lile Mungu alilofanya na Abrahamu?

Agano la Sinai lilikuwa kwa hali ya mambo ya kutunza Torati ya Musa; lile la Abrahamu lilikuwa ni kwa ahadi.

Kutoka 24: 3-8; Wagalatia 3:18.

**ISRAELI KATIKA JANGWA** *(Israel in the Wilderness)*

81) Israeli waliongozwa vipi kwa njia ya jangwani na Mungu? Ulianza lini huu mwongozo nao uliisha lini?

Kutoka 13: 21, 22. Kumbukumbu la Torati 31: 15.

82) Taja tukio la Ndama wa Dbahabu na walichofanya Musa na Haruni kwa jambo hilo.

Kutoka 32.

83) Toa maelezo ya kuwatuma wapelelezi 12 na tokeo la habari kwa Israeli. Kwa matokeo Mun gu alichua hatua gani juu ya taifa?

Hesabu 13 - 14.

## UTUMWA WA ISRAELI NA KUKOMBOLEWA KUTOKA KWA WAMISRI

*(Israel's Escape From the Slavery Under Egyptian Rule)*

Baada ya kuona jinsi ahadi za Mungu na agano lake kwa Abrahamu, Isaka na Yakobo utimilifu wake unapatikana kwa Bwana Yesu Kristo na kazi ya Kristo aliyoifanya, tunatazama tena kwa kifupi kipindi kilichokati ya "Mababa" na kuja kwa Yesu mara ya kwanza. Kipindi hiki ni mzunguko wa wa historia ya Agano la Kale, ambacho kinashughulika na mambo yanayowahusu wana wa Israeli—utumwa katika nchi ya Misri; kukombolewa kwao na mkono wa Musa; Agano la Mlima Sinai; Kuzunguka Jangwani; na kutwaa nchi ya Kanaani; kipindi cha Waamuzi; kuanzishwa kwa ufalme uliokuwa chini ya Daudi na Sulemani; kutengana kwa Israeli na Yuda; na hatimae kuangushwa na kutawanyika; na nusu kurudishwa, kwanza chini yake huyo Zerubbabeli, na halafu chini ya Ezra na Nehemia.

Wanafunzi wengi watajua mambo mengine kwa matukio haya kutoka kwenye masomo wanayoyapokea au kujifunza katika Shule ya Jumapili au (Sunday School lugha tunayoitamka mara nyingi), hivyo basi jambo moja moja sio lazima likumbukwe kwa kipindi hiki. Maswali yanayofuata yamepangwa kwa kuzunguka mambo yaliyojitokeza katika historia hii, nayo yatatumika na kuwa kama muhutasari wa yale yaliyofundishwa. Maswali yasipoeleweka au kufahamika kwa upande wa watoto, kwa kweli waalimu waongeze ziada kwa kufunza na kusahihisha.

Sura za kunukuu tu ndizo zimetolewa, mafungu ya maneno yakumbukwe kwa sehemu yanapohitajika. Mambo halisi ya kunukuu. yakumbushwe, kwa mfano, Amri Kumi, na madondoomakuu. katika Agano lililofanywa kwa Daudi. Haya yatatajwa kwa kunena au kuandika wakati wa kupita.

71) Mungu alimfunulia kitu gani Abrahamu kuhusiana historia ya wazao vake Wana wa laraeli ambayo ilikuwa iuafuata?

Mwanzo 15 : 13-17

72) Ni taifa gani la kigeni lililowatumikisha wana wa Israeli, na ni jinsi gani jambo hili lilianza?

Mwanzo 39 - 50; Kutoka 1-2.

73) Kwa mkono wa nani walikombolewa na Mungu kutoka Misri? Toa maelezo mafupi ya maisha ya kwaaza ya Muaa.

Kutoka 2-3.

74) Taja mapigo kumi ya Misri, na matokeo yake kwa Farao n» na Misri.

Kutoka 7-12.



52) Ni vipi wale ambao hawahusiki?

Wanakufa na kusahaulika kana kwamba hawakuwepo.

"Atakwenda kwenye kizazi cha baba zake; kamwe hawataona nuru" (Zaburi 49:19).

"Watalala usingizi wa milele wasiamke" (Yeremia 51:57).

"Wao wamekufa, hawataishi; wamekwisha kufariki, hwatafufuka; kwa sababu hiyo umewajilia, na kuwaangamiza, na kuupoteza ukumbusho wao" (Isaya 26:14).

53) Wenye haki kati ya wanaohusika watapokea nini kutoka kwa Kristo?

Kutokuharibika. Miili yao ya kufa itabadilika kwa muda mfupi kwa uweza wa Roho wa Mungu.

"Ataubadili mwili wetu wa unyonge, ili uweze kufanana na mwili wake wa utukufu" (Wafilipi 3:21).

"Sisi sote tutabadilika, kwa kitambo, kufumba na kufumbua jicho … Huu wa kufa uvae kutokufa" (1 Wakorintho 15:53).

"Tunatamani sana kuvikwa kao letu litokalo mbinguni … ili kitu kipatikanacho na mauti kimezwe na uzima" (2 Kor. 5:2-4)

"Mungu atatoa uzima wa milele kwa ambao kwa saburi katika kutenda mema wanatafuta heshima na kutokuharibika, watapewa uzima wa milele" (Rumi 2:7).

"Apandaye katika roho, atavuna katika roho uzima wa milele" (Wagalatia 6:8).

54) Watapatwa na nini wale atakao wakataa?

Wataondoka mbele zake kwa aibu, na kupata uchungu kama Jaji (Mwamuzi) atakavyo amua, na mwishowe kukoma kuwepo.

"Itakuwa kulia na kusaga meno, wakimuona Ibrahimu, Isaka na Yakobo na manabii wote katika Ufalme wa Mungu, ninyi wenyewe mkitupwa nje" (Luka 13:28).

"Wengine kwa aibu na kudharauliwa milele" (Danieli 12:2).

"Bwana Yesu atafunuliwa toka mbinguni katika mwali wa moto, na kuwalipa kisasi wale wasiomjua Mungu na wasio itii injili wa Bwana wetu Yesu Kristo: wataadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake" (2 Wathesalonike 1:7-9).

**UFALME WA MUNGU** *(The Kingdom of God)*

Tumeona kwamba Injili inayo "mambo yanayohusu Ufalme wa Mungu na Jina la Yesu Kristo". Kwa kifupi tumeona Jina la Yesu Kristo. Na sasa tunapima kuhusu ufalme wa Mungu.

55) Ufalme wa Mungu ni nini?

Ni ufalme ambao Mungu atausimamisha duniani nao utakuwa badala ya hizi falme zingine zote.

"Na katika siku za wafalme hawa Mungu wa mbinguni atausimamisha huo ufalme ambao hauti angamizwa kamwe … utazivunja vipande vipande falme hizi zote, nao utasimama milele na milele" (Danieli 2:44).

"Nitakipindua kiti cha enzi cha Falme na kuziharibu nguvu za falme za mataifa" (Hagai 2:22).

"Naye (Mwana wa Adamu) akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie" (Dan. 7:13-14).

"Naye Bwanan atakuwa mfalme wa dunia yote. Katika siku ile jina lake litakuwa moja na Bwana mmoja" (Zekaria 14:9).

"Malaika wa saba akaipiga baragumu, pakawa na sauti kuu katika mbingu zikisema, Ufalme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atamiliki hata milele na milele" (Ufunuo 11:15).

56) Ni nani atakuwa Mfalme katika Ufalme wa Mungu?

Yesu Kristo.

"Hawa wote wanatenda mambo yaliyo kinyume na amri za Kaisari, na kusema kuwa yupo mfalme mwingine, aitwaye Yesu" (Matendo 17:7).

"Mungu amepanga siku atakayo wahukumu walimwengu kwa haki kwa mtu aliye mchagua" (Matendo 17:31).

"Bwana atamiliki katika mlima sayuni tangu sasa na hata milele" (Mika 4:7).

"Falme za dunia hii umekuwa ni Ufalme wa Bwana wetu, na wa Kristo wake: naye atatawala milele na milele" (Ufunuo 11:15).

"Nami nimemuweka mfalme wangu juu ya mlima wangu mtakatifu Sayuni" (Zaburi 2:6).



"Wewe utamtimilizi kweli yako Yakobo, na Abrahamu rehema zako, ulizowaapia baba zetu tangu siku za kale" (Mika 7: 20).

"Na kwa habari ya wafu ya kwamba wafufuliwa: hamja soma katika kitabu cha Musa, jinsi katika kijiti Mungu alivyonena naye, akisema,. Mimi ni Mungu wa Abrahamu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo?" (Marko 12: 26).

"Ninyi mtamuona Abrahamu, Isaka na Yakobo na manabii wote katika Ufalme wa Mungu" (Luka 13: 28).

"Wengi watakuja kutoka mashariki, na kutoka magharibi, nao watakaa pamoja na Abrahanu, Isaka, na Yakobo, katika Ufalme wa Mbinguni" (Mathayo 8: 11).

70) Ni sehemu gani Bwana Yesu K risto— "MZAO" wa Abrabamu— atahusika katika utimilifu wa ahadi hizi zilizofanywakwa "Mababa" wa taifa la Wayahudi?

Ndiye aliyepangwa na Mungu kutimiza ahadi hizi; atarudi duniani kutoka mbinguni, kuwafufua na kuhukumu wafu, kusimamisha Ufalme wa Mungu hapa duniani, kutawala ulimwengu kwa haki akisaidiana na watakatifu waliokombolewa, na kuleta baraka kwa wakazi wa dunia kwa utawala wake mzuri wenye faida, utawala utakaodumu kwa miaka elfu. Abrahamu, Isaka, naye Yakobo wakiisha kufufaliwa na Yesu, watafurahia milki ya milele yanchi ya Kanaani waliyoahidiwa na Mungu.

"Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomuona akienda zake mbinguni" (Matendo 1: 9-11).

"Bwana Yesu Kristo atawahukumu walio hai na waliokufa atakapo funuliwa na ufalme wake" (2 Timotheo 4:1).

"Maana imempasa amiliki yeye, hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake" (1 Wakorintho 15:25).

"Nao (waaminifu na watakatifu wasiopatikana na mauti) wakawa hai, wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu" (Ufunuo 20: 4).

"Nanyi mtamuona Abrahamu, Isaka, na Yakobo ... katika Ufalme wa Mungu"(Luka 13 : 28).

"Siku ile Bwana akafanya agano na Abramu, akasema, Uzao wako nimewapa nchi hii, kutoka mto wa Misri, hadi ato mkubwa, Prati" (Mwanzo 15 : 18).

66) Ni "Mzao" gani ambao utatimiza hatinae hizi ahadi?

Ni Bwana Kristo.

"Basi ahadi ziliaeawa kwa Abrahaau na mzao wake. Hasemi, kwa wazao kana kwamba ni wengi; bali kana kwamba ni mmoja, na kwa mzao wako, ambaye ni Kristo" (Wagalatia 3 : 16).

67) Je! Mungu alifanya ahadi na agano na wengine mbali ya Abrahamu?

Ndiyo, kwa mwanawe Abrahamu, Isaka; na kwa mwana wa Isaka, Yakobo.

"Bwana alimtokea Isaka, akasema, Nitakupa wewe na uzao wako nchi hizi zote ... Na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watabarikiwa" (Mwanzo 26: 2, 4).

"Nchi hii uilalayo wowe (Yakobo), nitakupa wewe, na uzao wako" (Mwanzo 28: 13-14).

"Agano alilofaaya na Abrahamu, na uapo wake kwa Isaka, nalo alimthibitishia Yakobo" (Zaburi 105: 9).

68) Abrahamu, Isaka, na Yakobo waliimiliki nchi ya Kanaani waliyoahidiwa?

Hapana; walikuwa ni wageni katika nchi ya ahadi kwa kipindi cha uhai wao nao walikufa (wote watatu walizikwa Hebroni) pasipo kuipokea.

"Hawa wote walikufa katika imani, bila kuzipokea zile ahadi, bali waliziona tokea mbali na kuzishangilia, na kukiri kuwa walikuwa wageni, na wasafiri juu ya nchi" (Ebra. 11: 13-15, 39, 40). "Naye (Mungu) hakumpa (Abrahamu) urithi hata kiasi cha kuweka mguu: lakini akaahidi kuwa atampa, iwe miliki yake" (Matendo 7: 5).

"Kwa imani Abrahamu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka asijue aendako. Kwa imani alikaa ugenini ile nchi ya ahadi, kama katika nchi isiyo yake, akakaa katika hema pamoja na isaka na Yakobo, warithi wa pamoja naye wa ahadi ile ile" (Ebra, 11: 8-9).

69) Je! Mungu atatimiza ahadi yake kwa Abrahamu, Isaka, na Yakobo, kwa kuwapa nchi ya Kanaani, nchi waliyoikaa kama wageni wakati wa siku zao walipokuwa duniani?

Hakika Mungu atatimiza ahadi zake. Atamfufua Abrahamu, Isaka, na Yakobo toka wafu, na kuwapa waimilki nchi, hapo Ufalme wa Mungu utakaposimama Israeli ukiwa chini ya uongozi wa Bwana Yesu Kristo.



57) Je! Kristo atatawala peke yake Ufalme wa Mungu, au wengine watamsaidia?

Watakatifu watatawala pamoja naye.

"Kama tukiteswa, tutatawala pamoja naye" (2 Tim. 2:12).

"Umetufanya kwa Mungu wetu wafalme na makuhani: nasi tutamiliki katika dunia" (Ufunuo 5:10).

"Tazama, mfalme atatawala kwa haki, na wakuu kwa hukumu" (Isa. 32:1).

"Njoni, ninyi mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme" (Math. 25:34).

"Majira yakawadia watakatifu waumiliki ufalme" (Danieli 7:22).

"Watakatifu wa Aliye Juu wataupokea ufalme, na kuumiliki milele" (Dan. 7:18).

"Hamjui ya kuwa watakatifu watauhukumu ulimwengu?" (1 Kor. 6:2).
"Kufanya kisasi juu ya mataifa, na adhabu juu ya kabila za watu … heshima hii wanayo watakatifu wake wote" (Zaburi 149:7-9).

"Katika ulimwengu mpya (vitu vitakapo fanywa upya) Mwana wa Adamu atakapo keti kwenye kiti cha utukufu wake, nanyi mtaketi katika viti kumi na mbili, na kuhukumu kabila kumi na mbili za Israeli" (Math. 19:28).

58) Watakatifu ni nani?

Neno "mtakatifu" Maana yake ni mtu aliyetakaswa, au aliyetengwa na Mungu kwa imani ya kutii injili, na ambaye kwa uaminifu anafuata mfano wa Yesu Kristo.

"Kwa kanisa lililoko Korintho, wale waliotakasewa katika Kristo Yesu, walioitwa wawe watakatifu" (1 Kor. 1:2).

"Aliyewaita ninyi kwa injili yetu, ili kuupata utukufu wa Bwana wetu Yesu Kristo" (2 Wathesalonike 2:14).

"Kwa watakatifu walioko Efeso, wanaomwamini Kristo Yesu … ambaye mmemwamini pia baada ya kupokea neno la kweli, injili ya wokovu wenu" (Efeso 1:1,13).

59) Je! Mungu aliwahi kuwa na ufalme hapo awali duniani?

Ndiyo; Ufalme wa Israeli ulikuwa ni Ufalme wa Mungu, hasa Daudi na mwana wake Sulemani walipokuwa wanatawala.

"Israeli alipotoka Misri … Yuda ilikuewa patakatifu pake, na Israeli miliki yake" (Zaburi 114:1-2).
"Na sasa mwadhania mtauzuia ufalme wa Bwana mikononi mwa wana wa Daudi" (2 Mambo ya Nyakati 13:8).
"Ndipo Sulemani akaketi kwenye kiti cha enzi cha BWANA akiwa ni mfalme badala ya Daudi baba yake" (1 Mambo ya Nyakati 29:23).

60) Zamani huo Ufalme wa Mungu ulipatwa na nini?

Mungu aliupindua kwa sababu ya uovu, nao umebakia hali hiyo tangu hapo.

"Nitakipindua, pindua, pindua hiki, nacho hakitakuwapo tena mpaka ambaye ni haki yake nami nitampa" (Ezek. 21:25-27).
"Wana wa Israeli watakaa kwa muda wa siku nyingi bila kuwa na mfalme, wala mkuu, wala sadaka, wala nguzo …" (Hos. 3:4).
"Yerusalemu utakanyagwa na mataifa mpaka majira ya watu wa mataifa yatakapo timia" (Luka 21:24).

61) Ufalme wa Mungu, ambao Kristo na watakatifu watatawala, je! utakuwa na uhusiano wowote na ufalme wa Israeli uliokuwepo zamani?

Ufalme wa Israeli utarudishwa na kufanya uwe kitovu cha ufalme wa Mungu ujao na kushika ulimwengu mzima. Yerusalemu utakuwa ni makao makuu ya ufalme huo, ambao Yesu Kristo atautawala, sio tu akiwa Mfalme wa Wayahudi ambao watakuwa wamekusanywa katika nchi yao ya Israeli, bali akiwa Mfalme wa dunia yote.

"Atawakusanya watu wa Israeli waliotupwa, na kuwaweka pamoja watu wa Yuda waliotawanyika kutoka ncha nne za dunia" (Isa. 11:12).
"Nitawatwa wana wa Israeli toka kati ya mataifa walikokwenda; nami nitawakusanya pande zote, na kuwaleta katika nchi yao wenyewe, NAMI NITAWAFANYA KUWA TAIFA MOJA katika nchi hiyo, juu ya milima ya nchi ya Israeli; na MFALME MMOJA atakuwa mfalme wao wote; wala hawatakuwa mataifa mawili, wala hawatagawanyikana kuwa falme mbili tena, hata milele" (Ezekieli 37:21-22).

"Aliyemtawanya Israeli ATAMKUSANYA, na kumtunza, kama mchungaji afanyavyo kwa kundi lake" (Yeremia 31:10).
"Nitarejeza waamuzi wako kama walivyokuwa hapo mwanzo, na washauri wako kama hapo mwanzo" (Isaya 1:26).
"Katika siku hiyo nitaiinua maskani ya Daudi iliyoanguka, na kuziba mahali palipobomoka; nami nitayainua magofu yake, na kuyajenga kama siku za kale" (Amosi 9:11).
"Sheria itatoka Sayuni, na neno la Bwana toka Yerusalemu" (Mika 4:2).
"Atakuwa na mamlaka toka bahari hadi bahari, na toka mto hadi miisho ya dunia. Naam, wafalme wote watamsujudia; na mataifa yote yatamtumikia" (Zaburi 72:8,11).



## ABRAHAMU, ISAKA, NA YAKOBO "MABABA" WA TAIFA LA WAYAHUDI

*(Abraham, Isaac, and Jacob – The Fathers of the Jewish Nation)*

Kabla ya kuona maelezo zaidi yote ya utukufu wa ufalme wa Mungu utakaosimamishwa duniani Yesu atakaporudi, yatupasa kujifunza zaidi kuhusiana na taifa la Wayahudi ambalo ni mashuhuri sana kwa Mungu akishughulika na wanadamu. Kwa sababu hiyo tunarudi mwanzo kabisa wa taifa hili na kuona kile Biblia isemacho.

62) Abrahamu alikuwa ni nani?

Asili ya mtu huyu aliishi katika nchi ya Wakaldayo kwenye mji uliokuwa unajulikana kwa jina Uru, nao ulikuwa si mbali na Mto Frati katika eneo la Mesopotamia, lakini alipofikia umri wa miaka 75, Mungu akamwamuru yeye ahame, akawaacha rafiki zake na kuhamia katika nchi ya Kanaani.

"Mungu wa utukufu alimtokea baba yetu Abrahamu, alipokuwa katika Mesopotamia, kabla hajakaa Harani, akamwambia, Toka katika nchi yako, na katika jamaa zako, ukaende mpaka nchi nitakayo kuonyesha" (Matendo 7:2-3; Mwanzo 12:1).

63) Kwa nini Mungu alimwamuru Abrahamu ahamie Kanaani?

Kwa sababu ya kusudi alilolifanya kwake na kuhusu dunia yote, na kumfanya awe taifa kubwa; kwa Abrahamu na "uzao" wake mataifa yote yaweze kubarikiwa. Katika ahadi hii "injili" ilihubiriwa kwa Abrahamu.

"Nitakufanya wewe (Abrahamu) kuwa taifa kubwa … na jamaa wote wa dunia kwa njia yako watabarikiwa" (Mwanzo 12:2-3).
"Katika uzao wako mataifa yote ya dunia yatabarikiwa" (Mwanzo 22:18).
"Na Andiko, kwa vile lilivyoona tangu zamani kwamba Mungu atawahesabia haki mataifa kwa imani, lilimhubiri habari njema Abrahamu zamani, na kusema, Katika wewe mataifa wote watabarikiwa" (Wagalatia 3:8).

64) Ni ahadi gani zaidi ambayo Mungu alifanya kwa Abrahamu?

Mungu alimwahidi Abrahamu na "uzao" wake ahadi ya milele kumiliki nchi ya Kanaani, imeitwa Palestina na Nchi Takatifu.

"Nchi yote unayoiona (Abrahamu) nitakupa na uzao wako milele. Inuka, utembee katika mapana yake na marefu: kwa maana nitakupa wewe" (Mwanzo 13:15)

65) Ni kwa njia gani Mungu anatia nguvu kwa ahadi alizoawahidi Abrahamu?

Alifanya Agano na Abram na ni kweli atamtimizia hizi ahadi.